# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu*

TOLEO 1 | Septemba 7, 2022





# MAMA MALKIA

**Mama Ngina ndiye maana hasa ya 'nguzo ya mamlaka". Ameongoza maamuzi muhimu kwa enzi nne za urais – kutoka Mama Taifa hadi mama ya Rais wa nne.**

# COUNTY GOVERNMENT OF KAJIADO

**P.O BOX 11 – 01100, KAJIADO**

**KAJIADO COUNTY INVESTMENT AUTHORITY**

# ADVERTISEMENT OF VACANCIES

## POSITION; MEMBERS OF BOARD OF DIRECTORS

Kajiado County Investment Authority in collaboration with the County Government of Kajiado Invites interested persons with passion and vision to serve as members of the Board of Directors for a term of three (3) years.

**Requirements for Appointment**

1. Be a Kenyan Citizen;
2. Be a holder of a Bachelor's degree in economics, law, finance, accounting, or any business-related field from a University recognised in Kenya;
3. Have experience of at least ten years in senior level management in the public sector or private sector;
4. Demonstrates participation in local development initiatives;
5. Demonstrate excellent Interpersonal and communication skills;
6. Have the ability to work in a Multi-ethnic environment with sensitivity and respect for diversity;
7. Be a resident of Kajiado County.

**How to apply;**

Interested persons should **Hand Deliver** their application, Curriculum vitae and certified copies of academic testimonials, professional certificates, National Identity card and clearance certificates from Ethics and Anti-corruption Commission, Kenya Revenue Authority, Directorate of Criminal Investigations, CRB and Higher Education Loans Board to the undersigned on or before Thursday **13th September, 2022 5.00 p.m** in plain and sealed envelope marked 'Application for Board of Directors' to the address below.

**NOTE;**

- ONLY Shortlisted candidates will be contacted and they shall be required to produce original copies of the relevant documents;
- The County Government of Kajiado and Kajiado County Investment Authority is an equal opportunity employer and does not use agents nor does it charge any fees for employment;
- Youth, women, Persons living with Disability, marginalised and minority communities are encouraged to apply;
- Any form of canvassing shall lead to automatic disqualification;

**The County Secretary,**
**County Government of Kajiado,**
**P.O BOX 11 - 01100**
**KAJIADO.**

kauli ya mhariri

# Karibu kwa 'Darubini ya Wiki', nguzo ya uanahabari



Mutuma Mathiu

Hilary Ng'weno alirudi Kenya kutoka Chuo Kikuu cha Havard na kupata kazi kama ripota katika gazeti la 'Daily Nation.'

Alikuwa mwanahabari wa kipekee, mwenye uwezo mkubwa katika uandishi. Alifanya kazi kwa miezi tisa kabla ya kuteuliwa kuwa Mhariri Mkuu wa kwanza Mkenya katika gazeti hilo.

Aliwakilisha matumaini makubwa kwenye kizazi chake, hasa baada ya Kenya na mataifa mengi ya Afrika kupata uhuru.

Mafanikio yake yalionyesha dalili kwamba Waafrika wengi wangepata mafanikio mengi, hali iliyoandamana na matumaini yaliyokuwepo.

Kufikia wakati alipoanzisha gazeti la 'Weekly Review' (Darubini ya Wiki) mnamo 1975, matumaini yaliyokuwepo wakati wa uhuru yalikuwa yameanza kufifia. Viongozi Waafrika waliokuwa serikalini walikuwa wameanza kuonyesha sifa zao halisi - ukatili, mapendeleo na ukabila. Viongozi hao pia walianza kuonyesha tamaa kubwa.

Uzalendo uliokuwepo mwanzoni ukaisha na badala yake utawala mpya ukaanza kugeuka kuwa wa kiimla.

Gazeti la 'Weekly Review' lilikuwa la kipekee. Mpangilio wake uliangazia sifa za wahariri wake na hadhira iliyoilengwa. Hadhira yake ilikuwa ya watu walioelimika, werevu na waliokuwa tayari kuwakosoa viongozi waliokuwa mamlakani. Lilikuwa gazeti la watu wenye mitazamo huru; waliokuwa tayari kueleza mawazo yao kuhusu Afrika, licha ya hofu iliyotanda wakati huo kutoka kwa utawala uliokuwepo.

**Jarida la 'The Weekly Review' lililenga kuripoti, kufichua, kuelezea na kuonyesha athari za maamuzi, sera na matukio mengine. Lilijaribu kusaidia watu wenye mawazo pevu kung'amua yaliyokuwa yakiendelea katika jamii na matokeo yake kwa mtu binafsi. Ilidumisha ustawi wa demokrasia na haki za binadamu.**

Kabla ya kuanzishwa kwa 'Weekly Review', vyombo vya habari nchini wakati huo vilifuata mtindo wa vyombo vya habari Uingereza katika utoaji mafunzo kwa wanahabari. Wanahabari walianza kwa kufanya kazi ndogo ndogo katika chumba cha habari, lakini baadaye walifunzwa kuandika na kuhariri na watangulizi wao.

Mtu hakuwa akihitajika kuwa na kiwango cha juu cha elimu ili kuhitimu ama kuajiriwa kama mwanahabari. Sababu ni kuwa magazeti ya wakati huo yalikuwa yakiripoti matukio yaliyokuwa yamefanyika siku iliyotangulia kwa wasomaji wake.

Hata hivyo, Ng'weno aliajiri watu waliokuwa na shahada za digrii katika masuala kama fasihi. Kwa njia hiyo, alikuza mtindo wa kuangazia masuala tofauti kwa kina, badala ya kuripoti kama kawaida. Mtindo huo ulianza kuigwa na magazeti mengine.

Mtindo huo ulizua maswali kuhusu uhusiano wa matukio yaliyokuwa yakifanyika na athari zake. Vile vile ulijumuisha uchanganuzi wa matukio kwa upevu, bila mapendeleo yoyote.

Ni hali iliyokuza na kuboresha kiwango cha uanahabari nchini. Changamoto ya sasa ni kurejea nyuma miaka 47 iliyopita na kufufua tena mtindo huo; kuuboresha na kuufanya kukubalika kidijitali.

Toleo la kisasa ni daraja. Ni mahali ambapo kizazi cha hapo awali kitahisi kimefika nyumbani. Hata hivyo, tumefanya juhudi pia kukijumuisha kizazi cha sasa, ambacho hakijazoea au hakipendelei mtindo wa kueleza matukio ya hapo awali kwa njia ndefu.

Haya ni majaribio tu; itachukua muda kuleta usawa unaofaa.

Tunakukaribisha sana kuanza safari hii ya kubaini matukio mapya na kundi jipya la 'Darubini la Wiki.'

# Yaliyomo




**5 MKOSI WA RAILA:** Mkongwe wa siasa za Kenya ambaye ameponyokwa na kiti cha urais ambacho amegombea kwa jumla ya miaka 25 mfululizo. Je, safari yake ya Ikulu imefikia tamati?

**7 ASILI YA KORTI YA UPEO:** Kumekuwa na kesi tano za kupinga uchaguzi wa urais tangu 1997. Mnamo 2017, mahakama hiyo ilishangaza ulimwengu kwa uamuzi wake.

**18 NDOTO ILIYOTIMIA:** Mtengenezaji filamu chipukizi anabadilisha maisha ya vijana na kuelekeza macho ya dunia Kaunti ya Lamu kwa filamu zake zinashinda tuzo.

**22 HALI YA KIDINI:** TNyakati zimebadilika na ulingo wa kisiasa pia umebadilika. Lakini wajibu wa kanisa haujabadilika. Je, kanisa linatekeleza jukumu lake la kuhakikisha katika utawala?



Darubini ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu

**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji

**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Benjamin Situma, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

kurunzi ya Kenya


ENZI MPYA KENYA

# SAFARI NDEFU NA NGUMU

*Masaibu dhidi ya azma yake ya kuwa rais yalianza baada ya ushirikiano kati ya Rais Kenyatta na Bw Raila, maarufu kama 'handshake' ambao ulisababisha Naibu Rais kutemwa na mkubwa wake na hatimaye yeye na washirika wake kupigwa marufuku katika makao makuu ya Chama cha Jubilee.*

• Na BENSON MATHEKA

RAIS-MTEULE William Samoei Ruto, amevuka vizingiti vingi kuelekea uchaguzi alioshinda kuwa rais wa tano wa Kenya, na kuendeleza rekodi yake ya kutoshindwa tangu alipoanza kushiriki siasa za uchaguzi mnamo 1997. Vizuizi alivyovuka katika safari yake ya kuingia Ikulu vilitoka kwa mkubwa wake Rais Uhuru Kenyatta, kiasi cha kutengwa katika serikali ya chama cha Jubilee aliyokuwa Naibu Rais. Dkt Ruto alihimili upinzani na kutengwa serikalini kufuatia handisheki ya Rais Kenyatta na kiongozi wa ODM Raila Odinga mnamo Machi 9, 2018. Baada ya kutengwa serikalini pamoja na washirika wake hasa wabunge, kulifuatiwa na kufukuzwa katika chama cha Jubilee hadi akapigwa marufuku kukanyaga afisi za chama hicho tawala alichosaidia kuunda kabla ya uchaguzi wa 2017. Baadaye Rais Kenyatta alitangaza Bw Odinga kuwa chaguo la mrithi wake. Hii ilifanya maafisa wa serikali wakiwemo mawaziri, makatibu wa wizara na wakuu wa usalama kumdharau Dkt Ruto katika juhudi za kuzima azma yake. Washirika wake pia walipokonywa viti vya uongozi bungeni na Seneti ndiposa wakaungana kuunda chama cha United Democratic Alliance (UDA). Katika hatua nyingine ya kuzima azma ya Dkt Ruto, Rais Kenyatta na Bw Odinga walianzisha mchakato wa kubadilisha katiba kupitia Mpango wa Maridhiano (BBI) lakini mahakama zikauzima. Dkt Ruto alivumilia madharau na kejeli nyingi kutoka kwa washirika wa Rais Kenyatta na Bw Odinga walioapa kwamba hangekuwa kwenye debe katika uchaguzi mkuu. Hata baada ya kura kupigwa, maafisa wa serikali walijaribu kubatilisha ushindi wake kwa kushinikiza Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) lakini juhudi zao ziliambulia patupu. Kulingana na Bw Chebukati, kulikuwa na juhudi za kumzuia kumtangaza Dkt Ruto kuwa Rais-Mteule. Kizingiti cha mwisho ambacho alivuka ni kesi iliyowasilishwa katika Mahakama ya Upeo kupinga ushindi wake, ambao kwa mara ya kwanza katika historia ya Kenya, walalamishi tisa walipinga. Kesi hiyo iliyoamuliwa Jumatatu ambapo majaji saba wa mahakama hiyo walitupilia mbali kesi hiyo na kumthibitisha kuwa Rais – Mteule. Dkt alizaliwa mnamo Desemba 21, 1966, katika familia ya Bw Daniel Cheruiyot na Bi Sarah Cheruiyot. Alisomea Shule ya Msingi ya Kerotet kabla ya kujiunga na Shule ya Upili ya Wavulana ya Wareng Kapsabet. Alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi ambako alihitimu shahada ya digrii mwaka wa 1990. Alimuoa mkewe, Rachel Chebet mnamo 1991 na wamejaliwa watoto sita. Alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi ambako alihitimu shahada ya digrii mwaka wa 1990. Alimuoa mkewe, Rachel Chebet mnamo 1991 na wamejaliwa watoto sita. Alihudumu kama Waziri Msaidizi katika serikali ya Daniel Moi na kama Waziri wa Kilimo na Waziri wa Elimu ya Juu katika serikali ya Mwai Kibaki. Mnamo Agosti 15, Ruto alitangazwa Rais-Mteule na Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Wafula Chebukati baada ya kupata kura 7,176,141 (asilimia 50.59) dhidi ya mpinzani wake mkuu Raila, ambaye alipata kura 6,942,930 (asilimia 48.85). Lakini ushindi wake ulipingwa na Raila katika Mahakama ya Upeo na kusababisha kesi iliyoamuliwa Jumatatu ambapo majaji saba wa mahakama hiyo walitupilia mbali kesi hiyo na kumthibitisha kuwa Rais – Mteule.



# ALIVYOJIPANGA DHIDI YA UHURU NA RAILA

• Na MWANGU MUIRURI

Kwa Dkt William Ruto, kuwa Rais wa tano wa Kenya ni sawa na ndoto iliyogeuka ukweli.

Septemba 13, ataapishwa kuwa Rais wa tano wa Kenya. Kilicho wazi kumhusu Dkt Ruto ni kuwa hakuwa mwanasiasa wa kawaida.

"Baadhi yetu tuliotangamana naye katika miaka tisa iliyopita tulipoungana kuunda serikali ya Jubilee tunamfahamu kuwa mtu mwenye mipango mahsusi kwake binafsi na kwa washirika wake. Ni mweledi wa kimawazo na wakati fulani nilifikiria angefaa zaidi kuwa mwanajeshi," akasema Mwakilishi wa Kike Nyandarua Faith Gitau.

Mbunge wa Kandara, Alice Wahome, anasema: "Ruto anaweza kulia akifikiria anaweza kushindwa kuongoza wafuasi wake kufikia lengo lao…. Ilipobainika hatungeweza kuendelea kubakia katika Chama cha Jubilee, aliahidi kututafutia chama kipya na kwamba kitakuwa maarufu zaidi katika miaka miwili."

Anasema washirika wengi wa Ruto katika Jubilee hawakuamini jinsi angeweza kutimiza lengo hilo, lakini "alicheka tu, akisema anamwamini Mungu asiepungukiwa."


Mbunge wa Naivasha, Jayne Kihara, aliyewakaribisha Rigathi Gachagua, Moses Kuria, Ndindi Nyoro na Bi Wahome nyumbani kwake Naivasha Machi 21, 2018, kupangana jinsi ya kukabiliana na ushirika wa Bw Raila Odinga na Rais Uhuru Kenyatta kupitia 'handshake', alisema Dkt Ruto "ni mtu mwenye subira lakini katika kunyamaza kwake huwa anaona, kufikiria na kupanga vizuri."

Wakati wa kampeni zake, Ruto alionekana kujua vyema shabaha yake. Alifahamu kuwa adui wake mkubwa ulikuwa muungano wa Azimio la Umoja – One Kenya, ukiongozwa na Uhuru na Raila na kuungwa mkono na washirika mabilionea.

"Mikakati aliyotupa Dkt Ruto kutekeleza ilikuwa rahisi: Kukabiliana na mwenyekiti wa Azimio katika Mlima Kenya, kudhalilisha mradi wake (Odinga) na kumnyima kura katika ngome zake asili. Akiwa na Musalia Mudavadi na Moses Wetang'ula upande wake, alikuwa tayari kwa vita hivyo," akasema mwanachama wa kundi lake la kampeni.

■ BAHATI MBAYA

● Na MACHARIA GAITHO



# NI MWISHO WA RAILA KISIASA?

*Baada ya kugombea urais mara tano bila kufaulu, huenda wakati wa mkongwe huyu wa kisiasa kustaafu umewadia*

Baada ya Mahakama ya Upeo kumthibitisha Naibu Rais William Ruto kuwa rais – mteule wa Kenya, ni mara ya tano ya bahati mbaya kwa kiongozi wa Azimio, Bw Raila Odinga.

Raila, 77, ni mtetezi sugu wa demokrasia na haki za binadamu, ambaye mara tatu alikuwa mfungwa wa kisiasa wa serikali ya Moi.

Anatambuliwa wa kuongoza juhudi zilizoleta siasa za vyama vingi na kuzinduliwa kwa katiba mpya. Lakini baada ya kugombea urais mara tano bila kufaulu, huo huenda ukawa mwisho wa juhudi zilizoanzishwa na baba yake, marehemu Jaramogi Oginga Odinga, Naibu Rais wa Kwanza wa Kenya baada ya Uhuru na baadaye mpiganiaji siasa za vyama vingi nchini Kenya.

Raila, kiongozi mkongwe wa upinzani na nguzo ya siasa za maandamano, anajipata katika hali isiyo ya kawaida ya mgombeaji wa serikali iliyo mamlakani.

Aliungwa mkono na Rais Uhuru Kenyatta anayeondoka, ambaye alimtema naibu wake wa mihula miwili.

Wakati wa kampeni zake, Raila alilalamika kuhusu uwezekano wa kuhujumu uchaguzi, lakini akielekezea kidole cha lawama Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka badala ya serikali.

### Maisha ya utotoni

Raila alisomea Shule ya Msingi ya Kisumu Union na baadaye Shule ya Upili ya Maranda. Aliacha shule mnamo 1969 akasafiri Ujerumani Mashariki na kujiunga na Chuo cha Herder. Mnamo 1965, alipata msaada wa masomo katika Chuo cha Ufundi cha Magdeburg, kilichokuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Leipzig Ujerumani Mashariki.

Alihitimu kwa shahada ya Uhandisi mnamo 1970.

Aliporudi Kenya, alifanya kazi katika sekta ya umma kuanzia 1974 hadi 1982 alipotupwa kizuizini kutokana na shughuli zake za kisiasa.

Baadaye alishtakiwa kwa makosa ya uhaini na badala ya kesi yake kusikilizwa akatupwa kizuizini kwa miaka sita. Mama yake aliaga dunia mnamo 1984 Raila akiwa kizuizini.

Aliachiliwa mnamo Februari 6, 1988 kwa amri wa Moi, lakini akakamatwa tena Septemba mwaka huo na kutupwa kizuizini. Aliachiliwa Juni 12, 1989 kabla ya kutupwa ndani tena Julai 5, 1990, wakati huu akiwa na Bw Kenneth Matiba na Charles Rubia wakati wa kupigania demokrasia ya vyama vingi. Aliachiliwa Juni 21, 1991, lakini akakimbilia nchini Norway Novemba mwaka huo, akihofia kukamatwa tena.

Katika uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi mnamo 1992, Raila alishinda kiti cha eneobunge la Langata jijini Nairobi kwa tiketi ya chama cha Ford Kenya. Wakati huo, Ruto alikuwa mwanachama wa kundi la YK'92, akitafuta kuungwa mkono kisiasa na Moi.

### Mara ya kwanza ya kugombea urais

Katika Uchaguzi Mkuu wa 1997, Ruto alishinda kiti cha eneobunge la Eldoret North. Raila pia alishinda tena kiti cha Langata lakini kwa chama cha NDP kwa sababu alikuwa amegura Ford Kenya.

Raila pia alikuwa amegombea urais miongoni mwa wagombeaji wengine wakiwemo Mwai Kibaki (DP), Kijana Wamalwa (Ford-K) na Charity Ngilu (SDP).

Wenzake walipokuwa wakipinga ushindi wa Moi, Raila alibadilisha mbinu akaamua kushirikiana na Moi katika muhula wake wa mwisho chini ya katiba ya vyama vingi.

Ushirikiano huo ulipelekea NDP kumezwa na Kanu, ambapo Raila aliteuliwa Katibu Mkuu wa chama hicho tawala tangu 1963.

### Utengano na Moi, Kibaki

Mnamo 2002, Raila alitengana na Moi alipomuidhinisha Bw Uhuru Kenyatta kuwa mrithi wake. Raila na wanachama wengine wa Kanu, wakiwemo Kalonzo Musyoka, marehemu George Saitoti na marehemu Joseph Kamotho, walipinga hatua hiyo wakisema Uhuru, wakati huo akiwa na miaka 38, hakuwa na ujuzi wa kisiasa na uongozi wa serikali.

Walijiunga na chama cha Liberal Democratic Party (LDP), kabla ya kuungana na chama cha Kibaki cha National Alliance Party (Nak) na kuunda muungano wa National Rainbow Coalition (Narc) ambao hatimaye ulimshinda Uhuru katika Uchaguzi Mkuu wa 2002.

Baadaye alitengana na Kibaki na kugombea urais 2007 ambao ulikumbwa na ghasia mbaya zaidi kuwahi kutokea katika historia ya uchaguzi Kenya.

Aliteuliwa Waziri Mkuu kufuatia mashauriano ya amani yaliyoongozwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Dkt Kofi Anan. Uhuru na Mudavadi waliteuliwa naibu mawaziri wakuu naye Ruto akateuliwa Waziri wa Kilimo akiwa mwanachama wa ODM.

Lakini muda si mrefu Raila na Ruto walitofautiana. Ruto hakufurahia kwamba Mudavadi aliteuliwa Naibu Waziri Mkuu badala yake, ilhali alihisi alichangia zaidi kampeni za Raila.

Kwanza, Raila alimkasirisha Ruto kwa kuunga mkono kutimuliwa kwa watu katika Msitu wa Mau. Kisha akamlaumu kwa ufisadi katika Wizara ya Kilimo na kutangaza kuondolewa kwake hatua ambayo ilitekelezwa na Rais Kibaki.

Mambo yaliharibika kabisa 2007 Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) ilipochukua hatua kuhusu ghasia za uchaguzi mwaka huo.

Kiongozi wa mashtaka wa ICC, Luis Ocampo alipotoa orodha ya washukiwa, Raila kwanza alimtetea Ruto akisema alikuwa mwathiriwa.

Lakini hatimaye alibadili nia na kuunga mkono kesi za ICC dhidi ya Ruto na Uhuru, ambao walidaiwa kuwa viongozi wa ghasia hizo kutoka pande zote mbili.

Huenda Raila aliamini kuwa safari yake ya kuwa rais ingekuwa rahisi wapinzani wake hao wawili wakiondoka. Lakini mpango huo ulitibuka Uhuru na Ruto walipoungana, sio tu kupambana na kesi hiyo, bali pia kuitumia kuunda muungano mpya na wenye nguvu wa kisiasa kabla ya uchaguzi mkuu wa 2013.

### Chaguzi za 2013 na 2017

Muungano wa Jubilee ulishinda uchaguzi wa 2013, Raila akaambulia patupu kwa mara ya tatu.

Jubilee ilishinda tena 2017, Raila akakosa urais kwa mara ya nne.

Mwaka uliofuata Raila na Uhuru walibuni ushirika, sasa maarufu kama 'handshake' ambao hatimaye ulimfanya Uhuru kumtema Ruto na badala yake kumuunga mkono Raila.


Yaliyofuata, kama wanavyosema, ni historia.

**Amewahi kupata nafasi kadhaa za kutimiza ndoto yake ya kuingia Ikulu lakini kila mpango huo ulipoonekana kutimia ulitibuka ghafla.**

SIASA NA HAKI

# JINAMIZI LA UCHAGUZI KENYA

*Kila mwaka wa uchaguzi Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) imejipata katika njiapanda kutokana na shinikizo za viongozi wakuu wa mirengo tofauti ya kisiasa.*


Mohammed K. Ibrahim, 66



Naibu Jaji Mkuu Philomena Mwilu, 64


Jaji Mkuu Martha Koome, 62


Dkt Smokin Wanjala, 62


William Ouko, 60


Njoki Ndung'u, 56


Isaac Lenaola, 54

• Na MACHARIA GAITHO

Kile ambacho kingekuwa tukio la mpito katika uchaguzi wa urais wa 2017 katika Mahakama ya Upeo kilizindua mambo mengi kuhusu jinsi kesi hiyo hatimaye ilikamilishwa.

Naibu Jaji Mkuu Philomena Mwilu aliuliza ni kwa nini karatasi ya kura iliyopatikana katika sanduku lisilofaa ilifaa kuorodheshwa katika ujumuishaji wa mwisho wa kura zilizopigwa. Mawakili waliokuwa kortini wakiwakilisha washtakiwa wakuu - Rais Uhuru Kenyatta na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka - walitazamana kwa mshangao.

Mawakili hao walionekana kushangaa ni kwa nini jaji aliuliza swali kama hilo, lakini wakili mkuu aliyewakilisha IEBC aliposimama kufafanua, alianza kugugumiza. Mashauriano yalianza kwa minong'ono kati ya mawakili wa IEBC, na wakili mwingine aliyeamua kuelezea, naye pia akajipata kwenye mtego huku Jaji Mwilu akisisitiza kupewa jibu rahisi na la wazi.

Tabia za mawakili hao na mabadiliko ya nyuso zao zilionyesha mseto wa masuala ambayo yalipelekea kubatilishwa kwa matokeo ya uchaguzi wa urais, hatua iliyoweka historia ya uchaguzi nchini.

Suala lingine kuu mwaka wa 2017 lilikuwa kushindwa au kukataa, kwa IEBC 'Kufungua Sava'. Wakili mmoja alipoambia korti kwamba agizo la kuruhusu kuingia katika hifadhi ya matokeo ya uchaguzi halikuweza kutekelezwa kwa sababu, 'huko Ufaranza bado wanalala', ulikuwa mfano mwingine wa upuuzaji wa washtakiwa, ambao pia ulidhihirishwa na wakili mmoja aliyeonekana kulenga kutisha majaji wa Mahakama ya Upeo badala ya kutumia sheria na ushahidi katika kesi.

Hatimaye uamuzi huo wa kihistoria ulipotolewa na Jaji Mkuu wakati huo David Maraga, sababu ya kubatilisha ushindi katika uchaguzi wa Rais Kenyatta na Naibu Rais William Ruto haikuwa ushahidi wa kuongeza karatasi za kura, kuongeza idadi ya kura, kuvuruga ujumuishaji, udukuzi au kuingiliwa kwa mifumo ya tekinolojia ya IEBC na wageni, au ujanja mwingine ambao ungegunduliwa kwa urahisi kupitia kura kuhesabiwa upya na uchunguzi. Lilikuwa suala la mchakato. Mahakama ilipata kwamba IEBC haikuweza kueleza ilivyohesabu, kujumuisha kura na kupeperusha matokeo, na pia ilikwepa ilipotakiwa kufungua sava zake zipigwe darubini, kwa hivyo uwezekano kulikuwa na kitu ilichokuwa ikificha.

Kwa msingi huo pekee, badala ya ushahidi wa kutosha wa wizi wa kura, matokeo ya uchaguzi wa urais yalibatilishwa. Makosa yaliyotajwa na Mahakama ya Upeo yamekuwa jinamizi linalojirudia kwa makamishna wa tume ya uchaguzi. Kabla ya uchaguzi mkuu wa 2022, Mwenyekiti wa IEBC, Wafula Chebukati, alionekana kuamua kwamba badala ya kusubiri agizo la kufungua sava kesi ya kupinga matokeo ikiwasilishwa, angeziacha wazi kuanzia mwanzo. Kesi zilizowasilishwa na Raila na wengine kadhaa kupinga kutangazwa kwa Ruto kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais, ziliorodhesha sababu zinazofanana, lakini ni masuala machache muhimu yaliyojitokeza.

**Mwenyekiti wa IEBC Wafula Chebukati alijitihadi kuhakikisha Uchaguzi wa Agosti 9 ulionekana kuwa huru na wazi ili kuepuka malalamishi.**

Moja, ambalo lilifaulu 2017, ni kuhusu iwapo uchaguzi ulitimiza mahitaji ya kuwa huru, haki, kuaminika, kuthibitishwa na wazi. Sababu nyingine ni kwamba fomu za matokeo ya uchaguzi huo zilizoonyeshwa umma katika vituo vya kupigia kura, maarufu Fomu 34 A, hazikuwa mtandaoni. Hii ilipelekea sababu nyingine kwamba kulikuwa na udukuzi mkubwa wa tovuti ya IEBC ili fomu ambazo zilipakiwa mwanzoni, zibadilishwe au mpya kuwekwa badala yake. Pia, kulikuwa na malalamishi kwamba katika baadhi ya maeneo, uhesabu na ujumuishaji wa kura ulivurugwa na vile vile masuala kuhusu jinsi Chebukati alitamatisha ujumuishaji huku akiwatenga, ilivyodaiwa, wenzake wanne 'walioasi' na iwapo hesabu yake ilikuwa sahihi.

Majaji walipunguza kesi hadi masuala tisa pekee wayotumia kuamua lakini ngoma ilikuwa kwenye maelezo ya hati za viapo kadhaa. Moja ilikuwa kugawanyika kwa tume ya uchaguzi muda mfupi kabla ya makamishna wanne, Naibu-Mwenyekiti Juliana Cherera, Francis Wanderi, Irene Masit na Justus Nyangaya kukataa kuhusishwa na matokeo ambayo Chebukati alinuia kutangaza.

Katika hatua ambayo haikuwa imetendeka, makamishna 'walioasi' wa tume ya uchaguzi waliwasilisha majibu yao wakiunga ombi la Bw Odinga la kutaka matokeo ya uchaguzi yabatilishwe. Ni wazi kusema kwamba IEBC iligawanyika katikati, huku Chebukati, Profesa Abdi Guliye na Boya Molu wakiwa upande wa wachache dhidi ya Cherera, Wanderi, Masit na Nyangaya.

Kufikia wakati ambapo kesi iliwasilishwa, mgawanyiko huo ulikuwa umechukua misimamo huku Chebukati na kundi lake wakionekana kumtumikia Ruto, na kundi la Cherera likiunga mkono Raila. Hali itakuwa mbaya iwapo kesi itafaulu, na uchaguzi wa marudio kusimamiwa na tume iliyogawanyika.

Suala lingine moto lilikuwa madai ya Chebukati kwamba kundi kutoka kwa Kamati ya Taifa Kuhusu Ushauri wa Usalama lilijaribu kumshinikiza kubadilisha matokeo ya uchaguzi ili kumpendelea Raila. Ujumbe wao ulikuwa kwamba Kenya 'ingechomeka' iwapo Ruto angetangazwa mshindi wa uchaguzi wa urais, kwa hivyo, matokeo yalipaswa 'kukarabatiwa' kwa sababu za usalama wa taifa.

Iwapo ni kweli, athari zake zinaweza kudumu kwa muda mrefu hata baada ya uchaguzi na kuthibitisha madai ya Ruto kwamba serikali ya Uhuru Kenyatta ilipanga kutumia kila mbinu kumzuia kuwa rais.

ASILI YA KORTI YA UPEO

# SHERIA YAAMUA

*Kinara wa azimio alipata nafasi ya kubatilisha matokeo ya uchaguzi wa Agosti 9 lakini alishindwa kutoa ushahidi wa kutosha kuunga mkono malalamishi yake mbele ya mahakama.*

• Na OSCAR OBONYO

MVUTANO wa kisiasa ambao umeshuhudiwa nchini tangu uchaguzi wa Agosti 9, hatimaye ulisuluhishwa Jumatatu na Mahakama ya Juu kutokana na manufaa ya Katiba ya sasa na sheria bora za uchaguzi.

Ingekuwa miaka ya hapo nyuma, kesi hiyo, ambayo iliwasilishwa na mgombea urais wa Azimio la Umoja - One Kenya, Raila Odinga, ingetajwa tu mbele ya maafisa wa idara ya mahakama.

Isitoshe, kesi hiyo ingetupwa kwa misingi kuwa Bw Odinga na mgombea mwenza wake, Martha Karua, hawakufuata utaratibu unaohitajika.

Utaratibu huo ni pamoja na kumfikia Rais Mteule William Ruto na kumkabidhi yeye mwenyewe stakabadhi za kesi.

Hii ndiyo maana, kabla ya kuzinduliwa kwa Katiba ya sasa mnamo 2010, hakuna kesi ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa urais iliyowahi kufika hatua ya kusikizwa mahakamani mbele ya majaji.

Ingawa kesi yake ilitupwa, Bw Odinga alipata nafasi ya kuwasilisha tetesi zake kortini katika juhudi za kubatilisha matokeo ya uchaguzi wa urais wa Agosti 9.


Kesi hiyo, ambayo pia ilishirikisha kesi za walalalamishi wengine 10 kupinga ushindi wa aliyekuwa Naibu Rais William, ni ya tatu ya aina hiyo tangu 2010.

Dkt Otiende Amolo, wakili wa masuala ya kikatiba ambaye alihudumu kama mwanachama wa Kamati ya Wataalamu (CoE) walioandika Katiba hiyo ya 2010, anaeleza kuwa kuundwa kwa Mahakama ya Upeo kulilenga, miongoni mwa mambo mengine, kumpa nafasi mgombea urais asiyeridhika na matokeo kutafuta haki.

Mbunge huyo mteule wa Rarieda anaitazama mahakama hiyo kama asasi yenye nguvu ambayo tangu wakati huo, imepunguza mizozo ya kisiasa na kutoa matumaini kwa waathiriwa wa maovu ya uchaguzi.

Yamkini Otiende, ambaye ameshiriki mara mbili kesi za kupinga matokeo ya urais katika Mahakama ya Upeo na kufaulu, mnamo 2017, kubatilisha ushindi wa Rais Uhuru Kenyatta, ana uhafamu mkubwa.

Mahakama hiyo ambayo ilibuniwa chini ya Sura ya 10 ya Katiba, Kipengee cha 163 imetwika "wajibu wa kipekee wa kusikiza na kuamua kesi zinazohusu uchaguzi wa mshikilizi wa cheo cha Urais". Uamuzi kama huo, chini ya ibara ya 3, "utakuwa wa mwisho."



Kiongozi wa muungano wa Azimio la Umoja - One Kenya, Raila Odinga. Mahakama ya upeo ilitupa kesi yake ya uchaguzi.

Wakili Harun Ndubi anakubali kwamba Mahakama ya Upeo imeleta "kipindi cha utulivu" kati ya shughuli ya upigaji kura na fujo kutoka kwa wasioridhika.

Hata hivyo, wakili huyo, ambaye pia ni mtetezi wa haki za kibinadamu, anasema mahakama hiyo huendesha kazi zake chini ya makataa magumu, shinikizo na vitisho kutoka kwa wahusika.

"Hali hii huenda ikaathiri uwezo wa majaji wa Mahakama ya Upeo kuamua kesi kwa njia huru, haki na inayozingatia sheria," anasema.

Ndubi, ambaye alipinga ushindi wa Rais Kenyatta katika marudio ya uchaguzi wa urais 2017, anataja kisa ambapo mlinzi wa Naibu Jaji Mkuu, Philomena Mwilu, aliuawa kwa kupigwa risasi mchana peupe. Kisa hicho kilitokea Mahakama ya Upeo ilipokaribia kusikiliza kesi ya kupinga marudio ya uchaguzi wa urais Oktoba 26, 2017.

Baada ya mauaji hayo, karibu na jumba la Marsabit Plaza, barabara ya Ngong', aliyekuwa Jaji Mkuu David Maraga, alifika kortini akiwa ameandamana na Jaji Isaac Lenaola pekee. Alisema Mwilu alikuwa "ameingiwa na woga na mshtuko na hangefika."

Kupigwa risasi kwa mlinzi wa Mwilu kulijiri saa kadhaa baada ya kamishna mmoja wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Roselyn Akombe, kujiuzulu akidai maisha yake yalikuwa hatarini.

Hiyo ni kufuatia mauaji ya aliyekuwa Meneja wa Idara ya Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) wa tume hiyo, Chris Msando, siku tisa kabla ya Uchaguzi Mkuu Agosti 8, 2017.

Vitisho vya aina hiyo visipokomeshwa, Ndubi anasema wajibu mzuri ambao Mahakama ya Upeo inatekeleza "hautachukuliwa kuwa muhimu."

Wakili huyo anaongeza kuwa masilahi makubwa ambayo wadau wakuu wameweka katika uchaguzi wa urais pia ni tisho kubwa katika kupatikana kwa haki.

Ingawa, kwa kiwango fulani, Katiba inashughulikia changamoto hii kupitia mfumo wa utawala wa ugatuzi kupitia serikali za kaunti, watu wengi hawajabadilisha mtazamo wao.

Bado wameweka matumaini yao makubwa kwa urais.

Kabla ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Upeo, waliopoteza katika chaguzi mbalimbali, kwa kutendewa hiana, walitafuta haki katika mahakama za hadhi ya chini. Majaji na maafisa wengine wa mahakama hizi waliteuliwa moja kwa moja na rais.

Hiyo ni kinyume na sasa ambapo Katiba inaelezea utengano wa kimamlaka kati ya nguzo tatu za serikali - Serikali Kuu, Bunge na Idara ya Mahakama. Wakati huu, Tume ya Huduma za Mahakama (JSC) ndiyo inayoajiri majaji, mahakimu na maafisa wa asasi hiyo. Naye Rais huteua Jaji Mkuu baada ya tume hiyo kuwahoji waliotuma maombi na kupendekeza anayefaa kuteuliwa.

Picha ya Bi Karua akilumbana na Dkt Ruto katika jumba la KICC baada ya matokeo tata ya uchaguzi wa urais 2007 ingali kwenye mawazo ya wengi.

Akiangazia miaka ya nyuma, aliyekuwa Naibu Mwenyekiti wa iliyokuwa Tume ya Uchaguzi Kenya (ECK) Gabriel Mukele, anakubali kuwa ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007 zilisaidia uchaguzi.

"Kabla ya kurejelewa kwa mfumo wa utawala wa vyama vingi, chaguzi za urais ziliendeshwa vibaya ambapo mtetezi wa wadhifa huo ndiye aliibuka mshindi wa moja kwa moja," anasema.

Ingawa Raila amelaumiwa na wengi kwa "kukataa kushindwa" na "kuwasilisha kesi za kupinga matokeo ya urais kila mara," mawakili wamekubali kuwa kesi zake zimechangia kupatikana kwa mageuzi katika sheria za uchaguzi.

Aidha, kesi zake zimeimarisha uwezo wa mahakama kushughulikia kesi kuhusu masuala ya uchaguzi.

Juzi mahakama hiyo ilipata fursa ya kutoa uamuzi wake wa kipekee ambao mawakili wanaamini utasaidia kuboresha sheria za uchaguzi Kenya.

kurunzi ya Kenya

■ MWANAMKE MWENYE NGUVU ZAIDI KENYA

# NGUZO YA MAMLAKA YA UHURU

*Mbali na Kamanda Mkuu wa Vikosi vya Usalama Kenya, huyu hasa ndiyr bosi. Akiwa Mama wa Taifa katika ya 1963 na 1978, na baadaye 'Mama Rais' kutoka2013, Mama Ngina ni miongoni mwa watu wenye nguvu zaidi nchini. Wakati wa enzi za Jomo Kenyatta, mawaziri na maafisa wa serikali walijua tamko lake lilikuwa sheria.*

● Na MACHARIA GAITHO

Huku Rais Uhuru Kenyatta akielekea mwisho wa muhula wake wa pili kama rais wa Kenya, si mtu binafsi anayeondoka, lakini pengine mwisho wa familia yenye ushawishi mkuu katika siasa za Kenya.

Mbali na kuwa rais anayeondoka, mtu mwingine ambaye anaweza kuhisi amepoteza pakubwa ni mama yake, Mama Ngina Kenyatta, kiongozi wa familia hiyo, ambaye alihudumu kama Mama Taifa wakati wa utawala wa baba ya Uhuru, Mzee Jomo Kenyatta.

Tangu alipoingia katika maisha ya umma akiwa bi harusi mchanga wa shujaa wa vita vya uhuru aliyemzidi kwa umri, hakutamka neno mbele ya umma. Lakini akiwa Mama Taifa wa Kenya kati ya 1963 na 1978 na baadaye Mama wa Rais kutoka 2013, Mama Ngina ametambuliwa kama mmoja wa watu wenye nguvu nchini, na kwa njia nyingi kama mtu mwenye ushawishi mkubwa katika maamuzi ya uongozi.

Akiwa Mama wa Taifa, Mama Ngina alionekana akitabasamu huku akitembea hatua moja nyuma ya shujaa wa ukombozi. Alionekana kuwa mke aliyetekeleza majukumu yake, aliyeelewa vyema nafasi yake na asiyeweza kuingilia mumewe akishughulika na masuala ya serikali yaliyohusisha wanaume pekee.

Hata hivyo, mbali na kuonekana hadharani, mawaziri, wanasiasa na maafisa wengine wa serikali walijua kwamba katika Ikulu ya Nairobi; Ikulu za Mombasa na Nakuru ambako Rais Kenyatta alikuwa akitembelea; na pia katika boma la familia katika mji mdogo wa Gatundu, kilomita 50 nje ya Nairobi, ndiye alikuwa akiamua mambo.

Kenyatta huenda alionekana kama kiongozi wa Afrika mwenye nguvu ambaye hakuvumilia uasi wa kisiasa, na aliyeamini kuwa wanawake na watoto wanafaa kujua nafasi yao katika familia.

Hata hivyo, alimpa msichana aliyeoa kama mke wa nne akiwa na umri wa miaka 18 naye akiwa na zaidi ya miaka 50, usemi zaidi nyumbani.

Mumewe alipofariki mwaka wa 1978, aliacha majukumu ya Mama wa Taifa na kusimamia utajiri mkubwa wa familia. Alirudi katika maisha ya umma miaka 35 baadaye mnamo 2013 mwanawe wa kwanza wa kiume, Uhuru Muigai, alipofuata nyayo za marehemu kiongozi wa familia kwa kuchaguliwa Rais wa Kenya.

Hakurudi kuishi Ikulu au kutekeleza shughuli zozote za umma, huo ulikuwa wajibu wa Mama wa Taifa, Margaret, mpenzi wa Uhuru tangu utotoni. Lakini muda si mrefu iliibainika kuwa Mama Ngina aliendelea kuwa na ushawishi mkubwa kwa mwanawe, rais wa pili, katika maisha yake. Hakutaka kuonekana akizua mizozo wala hakuonekana hadharani. Lakini alikuwa mama kiongozi wa familia na kwa hilo alikuwa wa kwanza katika mpangilio wa itifaki kifamilia.



Mama Ngina Kenyatta, akiwa na mwanawe Uhuru Kenyatta, eneo la Gatundu.

Mara ya pekee aliyozua mzozo ilikuwa Machi mwaka huu alipoingilia tofauti kati ya Uhuru na Naibu Rais William Ruto, akimtaja Dkt Ruto kuwa mtu ambaye hakupata malezi bora.

Mama Ngina alikuwa akihutubia waombolezaji katika mazishi ya binamu yake eneo la Gatundu, alipozungumzia siasa akiambia umati kwamba kiongozi wao, mwanawe, aliwatakia mema watu wake kwa kumtema Ruto na kushirikiana na Kiongozi wa Upinzani Raila Odinga.

Kauli hiyo ilikuwa tofauti na wakati wa mwisho ambao Mama Ngina alitoa tamko kuhusu ushirikiano wa "UhuRuto". Huo ni wakati wa kabla ya uchaguzi wa 2013 katika mkutano uliohudhuriwa na watu wengi, pia eneo la Gatundu, alipojitokeza baada ya kutoonekana hadharani kwa muda, kubariki Uhuru na Ruto, ambao wakati huo walikuwa wakijiandaa kugombea urais kwa tikiti moja huku wakiandamwa na kesi katika Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa (ICC) kuhusu ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007.

Ruto alikuwa akinuia kugombea urais kwa mara ya kwanza mwaka wa 2013, lakini baada msururu wa mazungumzo yaliyochukua muda mrefu akakubali kujiondoa na kumuunga mkono Uhuru. Kilichomfanya akubali kuwa Naibu Rais wa Uhuru ni pesa. Ruto hakuwa na pesa kama walizo nazo familia ya Kenyatta kutumia katika kampeni za urais.

Mama Ngina ndiye aliyekuwa na ufunguo wa pesa hizo ambaye hata umri wake ukiwa mkubwa, anasimamia himaya kubwa ya biashara za familia hata kama hahusiki na shughuli za kila siku za usimamizi. Hata akiwa Rais, Bw Kenyatta aliachia mama yake na kaka yake mdogo mwenye ushawishi, Muhoho, kusimamia moja kwa moja biashara za familia ya Kenyatta. Ingawa kwa jumula anaonekana kutopenda siasa, Mama Ngina anajulikana kwa kuwa na usemi mkubwa.

Kwa mfano, Mzee Kenyatta alipokufa mwaka wa 1978, kiti cha ubunge cha Gatundu Kusini kilishikiliwa na mpwa wake aliyempenda, Ngengi Muigai, ambaye aliwakilisha maslahi ya familia katika bodi za mashirika tofauti. Uhuru na kaka yake Muhoho walikuwa wa umri mdogo wakati huo.

Ngengi Muigai alishinda kiti hicho katika uchaguzi mkuu wa 1983 lakini katika uchaguzi uliofuatia miaka mitano baadaye, akatofautiana na Mama Ngina baada ya kuripotiwa kumsuta. In-

kurunzi ya Kenya

# MAMA NGINA: MKONO FICHE

• Na JOHN KAMAU

Hakuna mwanamke yeyote Kenya ambaye amefurahia mamlaka kumshinda Mama Ngina Kenyatta. Licha ya hayo, mamlaka hayajawahi kumwingia kichwani. Ameona mamlaka yakiondoka na kurudi haraka katika boma lake lakini haonekani wala kusikika.

Kuanzia kuwa mkewe rais, hadi kuwa mama yake rais, Mama Ngina amegubika jukwaa la kisiasa nchini Kenya kama jitu.

Hadithi ya Mama Ngina bado haijaandikwa. Mtazamo wake kuhusu safari ya Kenya kisiasa haijulikani na umesalia kuwa makisio ya kihistoria.

Akiwa hadharani, Mama Ngina kila wakati amekuwa akionekana mtulivu na asiye na wasiwasi wowote. Iwapo anasheheni mamlaka yoyote, kwa kawaida huwa ni kupitia uhusiano – lakini bila shaka yeye ndiye nguzo ya familia kuu ya Kenyatta, ambayo imetawala Kenya kwa robo karne.

Hapendi kuangaziwa ila huwa hakosi kuhudhuria hafla ndogondogo za vijijini – ambako ni nadra kwake kujiingiza kwenye siasa – Tangu 1952, ambayo ni miaka 70 leo, Mama Ngina amefungamana na siasa za Kenya kama mlengwa, mshiriki, mwangalizi au kama mkono usioonekana.

Jina lake lipo kwenye mitaa ya miji mikuu, ufuo mmoja Mombasa unabeba jina lake na katika kijiji chake cha Gatundu, Chuo Kikuu cha Mama Ngina kinaelekea kuzinduliwa.

Mama Ngina ametazama tawala nne za marais kwa karibu na katika muda huo amekuza utajiri wa familia yake na kujenga himaya ya kutamaniwa.

Ajabu ni kuwa, ni nadra kwake kuanika utajiri wake, hana madaha, ilhali ni mmoja kati ya wanawake matajiri zaidi nchini Kenya, kulingana na Jarida la 'Forbes'. Miaka michache iliyopita, jarida la 'Venture' lilimuorodhesha kama mmoja kati ya mabilionea barani Afrika kutokana na uwekezaji wake katika sekta za benki, kawi, hoteli na malazi pamoja na ustawi. Kila jina lake linapotajwa vibaya, nguzo yake kuu imekuwa kunyamaza badala ya kujibizana na wanaomlenga.

Mama Ngina, akiwa binti ya Chifu Muhoho Gatheca, aliolewa na mmoja wa wanasiasa maarufu zaidi Afrika, Jomo Kenyatta, aliyeshika usukani wa siasa za humu njini baada ya kuishi Uropa kwa miaka 15. Ghafla, hata kabla ya kuhitimu umri wa miaka 20, Mama Ngina alikuwa amerushwa katikati ya siasa za Kenya enzi za ukoloni huku Jomo akizunguka kote nchini akitafuta kuungwa mkono kwa chama chake cha kisiasa, Kenya African Union (KAU) kilichojumuisha tawi lenye msimamo mkali la Jeshi la Kupigania Ardhi na Uhuru wa Kenya, Mau Mau.

Akiwa amenaswa katika harakati hizi za kisiasa, Mama Ngina alikuwa miongoni mwa waliolengwa kukamatwa katika msako ulisababisha Jomo kuzuiliwa wakati wa Hali ya Hatari mnamo 1950.

Vyombo vya habari Uingereza na walinzi wa magereza walimpa Mama Ngina lakabu nyingine: "mke wa gaidi." Pamoja na mtoto wake mchanga, Kristina, Mama Ngina alifungiwa katika Gereza la Kamiti msako mkali dhidi ya

endelea uk 23



**Rais Moi na Mama Ngina Kenyatta jijini Nairobi wakati wa sherehe ya ukumbusho wa miaka 18 tangu Mzee Kenyatta alipoaga dunia.**

asemekana Mama Ngina aliapa kumfunza adabu na akapeleka malalamishi yake kwa mrithi wa Rais Kenyatta, Daniel arap Moi. Kwa amri fupi tu, chini ya utawala wa chama kimoja, Moi alipokuwa akifanyia majaribio mfumo wake wa kupiga kura kwa mlolongo, Ngengi aling'olewa Bunge. Ni muhimu kufahamu kwamba Uhuru alipoingia katika siasa mwaka wa 1997 akigombea kiti cha 'familia', alishindana na kaka yake Ngengi, Kapteni Kungu Muigai, aliyejitwika kiongozi wa mojawapo ya mirengo ya Wazee wa Jamii ya Agikuyu, na ambaye sasa amejitenga na msimamo wa familia hiyo na kuunga azima ya urais ya Dkt Ruto huku akimfanyia kampeni.

Kungu na Ngengi ni wana wa ndugu wa kambo wa Rais Kenyatta, James Muigai, kwa hivyo inawezekana mzozo wa familia ulitokana na urithi wa mali ya mwanzilishi wa familia yao.

Dada yao, Seneta Beth Mugo, kwa upande mwingine, amekuwa mwandani na mshirika wa biashara wa Mama Ngina tangu miaka ya sabini. Isipokuwa uchaguzi mkuu wa 1988, Mama Ngina alikuwa akimtegemea Moi kwa njia nyingi. Rais Kenyatta alipokufa, aliacha utajiri mwingi ambao haukuwa umepangwa vyema, mwingi ukiwa ardhi iliyohamishwa kutoka kwa umiliki wa umma, lakini stakabadhi hazikuwa zimekamilika.

Alimtegemea Rais Moi kukamilisha uhamishaji na utoaji wa hati miliki. Hakuwa amesoma sana na watoto wake walikuwa bado shuleni.

Watoto wakubwa wa wake wa kwanza wa Mzee Kenyatta walikuwa pia wakitafuta urithi wao. Kutoka kwa Moi, Mama Ngina alijifunza kuajiri wasimamizi wataalamu, sio watu wa familia na jamaa, kuendesha biashara. Ni kwa sababu yake ambapo mali aliyorithi ilibadilika kuwa biashara kubwa za kisasa katika sekta za hoteli, benki, bima, kilimo, utengenezaji wa chakula, majengo, elimu na mashirika ya habari.

Mama Ngina alizaliwa mwaka wa 1933, akiwa binti wa chifu wa enzi za ukoloni, Muhoho wa Gathecha, kwa hivyo alikuwa na damu ya uongozi, ilhali Jomo Kenyatta, ambaye alimuoa mwaka wa 1951 alikuwa mtu kawaida. Alikuwa na umri wa miaka 18 naye Jomo alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 50 na tayari kiongozi wa vita vya ukombozi.

Mwaka mmoja baada ya kuolewa, mumewe alikamatwa na serikali ya wakoloni iliyotangaza Hali ya Hatari kutokana na kuzidi kwa mapigano ya Mau Mau. Aliachwa peke yake kutunza binti yake, Kristina Wambui, akiwa mchanga wakayi huo. Hakuungana na mumewe hadi 1960 alipomaliza kifungo cha miaka saba, lakini akabaki kizuizini katika sehemu pweke ya Kaskazini ya Kenya. Mama Ngina aliruhusiwa kumtembelea Kenyatta katika nyumba aliyozuiliwa Kapenguria, na huko ndiko alipata mimba ya mwanawe wa pili, Uhuru.

Uhuru alizaliwa 1961 akifuatwa na dada yake Anna Nyokabi mwaka wa 1963 na kaka yake Muhoho mwaka wa 1965. Kuendelea kwa Mama Ngina kuthibiti masuala ya kifedha ya familia kulidhihirika Oktoba mwaka jana kufuatia ufichuzi wa kwamba anamiliki akaunti ambazo zimefichwa pesa nyingi nchi ya ng'ambo ili kukwepa kulipa ushuru. Ufichuzi wa mali ya siri uliofanywa na Kundi la Wanahabari Wapekuzi Ulimwenguni uliorodhesha Mama Ngina kama mmiliki wa kwanza na Uhuru Kenyatta kama mmiliki wa pili.

Ingawa hakuna ushahidi wa makosa uliogunduliwa, akaunti za siri katika maeneo kama Panama, Switzerland, Bermuda, Jersey na Malta huwa za watu wanaotaka kuficha pesa haramu au kuficha utajiri wao usitozwe ushuru. Ufichuzi huo uliaibisha Uhuru, ambaye alikuwa akijionyesha kama rais aliyejitolea kupiga vita ufisadi. Alisema alikaribisha ripoti hiyo na akaahidi kutoa ufafanuzi zaidi akirudi kutoka ziara ya ng'ambo lakini hajawahi kutamka neno kuhusu suala hilo tangu wakati huo.

kurunzi ya Kenya

WALIVYOUNDA JARIDA SAFI

# WAPI WAASISI WA 'DW'?

*Orodha ya waliokuwa waandishi wa Darubini ya Wiki inaonyesha kuwa wengi wao walinawiri kwingineko. Wako wapi?*

• Na MUIRU NGUGI

WANAHABARI popote duniani huwa watu wakakamavu. Lakini waliofanyakazi katika "Darubini ya Wiki" (DW) wanahitaji sifa maalumu kwa bidii na ustahimili wao.

Katika miaka 24 ya kuchapishwa kwake, jarida la (DW), kama lilivyojulikana katika majukwaa ya uanahabari, lilikuza kundi la wanahabari wa kuheshimika, ambao walitoa mchango mkubwa katika nyanja tofauti kitaifa na kimataifa kutokana na bidii yao, ustadi wa kuandika na uchanganuzi wa kina wa matukio.

Jarida hilo ambalo lilizinduliwa mnamo Februari 1975 na Hillary Ng'weno, ambaye alisomea katika Chuo Kikuu cha Havard nchini Amerika, lilijikita katika uchanganuzi wa habari za siasa na biashara zilizojiri nchini Kenya, kwa undani na pasina kupendelea pamoja na ripoti za matukio muhimu barani Afrika.

DW lilitoa jukwaa ambapo watu wa tabaka hilo waliweza kufuatilia na kuchanganua masuala yaliyowahusu Wakenya.

Baadhi ya waandishi wa DW sasa 'wamerudi nyumbani' na ni miongoni mwa kundi la waandishi na wahariri ambao wamejitolea kufufua jarida hilo maarufu Kenya lililofungwa mnamo 1999.


Wanapoanza upya, wanalazimika kukumbatia masuala ya sasa, ikiwemo jamii iliyopitia mabadiliko mengi, wingi wa vyombo vya habari vya kawaida na visivyo vya kawaida na ambavyo mara nyingi hutoa habari za uongo kwa lengo la kupata faida.

Wanahabari hao mahiri ambao umri wao ni mkubwa pia wanalazimika kukabiliana na mabadiliko katika mpangilio wa vyumba vya habari.

Kwa bahati nzuri, wanahabari hao wa zamani sasa wanafanya kazi na wanahabari chipukizi wenye ujuzi mkubwa katika matumizi ya tekinolojia ya kisasa.

Mseto wa kizazi cha zamani cha wanahabari na wale wa kizazi kipya unalenga kuzalisha jarida lenye ubora wa kiwango cha juu.

Ni vigumu kuwapata wafanyakazi wote wa zamani wa jarida la DW, ambao walilistawisha kwa karibu robo karne. Haya hapa ni maelezo kuhusu wachache wao;



Hilary Boniface Ngw'eno, maarufu kama HBN alianzisha jarida la 'The Nairobi Times' na kituo cha kwanza huru cha Televisheni Kenya, STV.

Alitayarisha msururu wa makala kuhusu historia ya Kenya ikiwemo 'Making of a Nation' na 'Kenya's Darkest Hour'.

Aliaga dunia Julai 7, 2021 baada ya kuugua kwa muda mrefu na kuacha kumbukumbu ya ubora na ujasiri katika taaluma ya uanahabari.

Mmoja wa wahariri anayehusishwa na maendeleo, ufanisi na kuimarika kwa ubora wa DW alikuwa Sarah Elderkin, Mkenya mwenye asili ya Uingereza.

Alianza kama Katibu Mtendaji wa Hilary Ng'weno jarida hilo lilipozinduliwa na baadaye akapanda cheo kuwa Mhariri Msimamizi.

Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Cardiff, Uingereza kusomea shahada ya kwanza katika taaluma ya Uanahabari.

Philipi Ochieng', mmoja wa wahariri watajika Kenya, alifanya kazi kwa muda mfupi kama Mhariri Mshirika wa DW mwishoni wa miaka ya sabini.

Baadaye alijiunga na shirika la habari la Nation Media Group (NMG) ambako alinawiri kitaaluma na kuhudumu kama Naibu Mhariri Msimamizi.

Baadaye Ochieng' alifanyakazi kama Mhariri Mkuu wa gazeti la 'Kenya Times'. Aliaga dunia mwaka jana miezi michache kabla ya kifo cha mwenzake HBN.

Samuel Makinda aliyeandikia DW mwishoni wa miaka ya sabini, pia aliwahi kufanya kazi katika 'Daily Nation'.

Wakati huu ni Profesa wa Siasa na Masuala ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Murdoch, Australia.

Mwanahabari mwingine mwenye uzoefu mkubwa alikuwa Peter Kareithi, mweledi wa ukusanyaji wa habari ambaye sasa ni Profesa wa taaluma ya Mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Penn State, Amerika.

Ripota mpekuzi, Mutegi Njau, ambaye aliandika habari kuhusu kufungwa kwa DW katika 'Daily Nation' 1999 alifanya kazi katika Shirika la Royal Media Services kama mhariri kabla ya kustaafu miaka michache iliyopita.

Wachira Waruru alipanda cheo kutoka ripota hadi Mhariri Msimamizi wa DW kabla ya kuondoka mnamo 1993.

Baadaye alihudumu katika usimamizi akiwa Mkurugenzi Mkuu wa Mashirika ya Habari ya 'The Standard' na Kenya Broadcasting Corporation (KBC) kabla ya kutunikiwa cheo cha Afisa Mkuu Mtendaji wa Shirika la Royal Media Services.

Jaindi Kisero, mmoja wa waandishi bora wa masuala ya biashara, alihudumu kama Mhariri wa Habari za Biashara katika DW na baadaye akapanda cheo kuwa Mhariri Msimamizi.

Jaindi atakuwa akiandikia 'Darubini ya Wiki' iliyozinduliwa upya.

Macharia Gaitho alihudumu kama Naibu Mhariri Msimamizi wa DW hadi alipoondoka mnamo 1993 kuungana na Peter Warutere aliyefanya kazi naye katika jarida la 'The Economic Review'. Alihudumu katika wadhifa huo huo wa Naibu Mhariri Msimamizi.

Baadaye alijiunga tena na gazeti la 'Daily Nation' ambako alihudumu kama Mhariri Msimamizi wa Miradi Maalumu.

Mwandishi mwingine mkongwe, Gitau Warigi, alijiunga na 'Daily Nation' ambapo anaandikia safu ya maoni.

Ripota Mkuu Vitalis Musebe aliondoka DW na kujiunga na kituo cha televisheni cha KTN kama Mhariri wa Habari na baadaye akahudumu kama Mhariri Mkuu katika Shirika la Utangazaji Kenya (KBC).

Baada ya kuondoka DW, Kwendo Opanga aliendelea kuwa mmoja wa waandishi shupavu wa maoni Kenya.

Alianza kwa kuandikia 'Daily Nation' kabla ya kujiunga na 'The Standard' ambako alipanda cheo kuwa Mhariri Msimamizi.


McOwiti O. Thomas aliajiriwa kuwa mwandishi wa makala ya Sayansi katika DW. Baadaye alipata kazi katika Afisi za Umoja wa Mataifa (UN) jijini Nairobi. Aliondoka nchini na sasa anaishi Amerika. Atakuwa mmoja wa wachangiaji wa makala wa jarida hili.

Baada ya kutoka DW, Mwangi Githahu alifanya kazi katika magazeti ya humu nchini yakiwemo 'Kenya Times' na 'Star' kabla ya kuhamia nchini Afrika Kusini ambako anaishi na kufanya kazi.

Okumba Miruka, ambaye alihudumu kama mwandishi wa masuala ya sanaa na utamaduni ni mshauri wa masuala ya jinsia na maendeleo kando na kuwa msomi.

Okodan Akwap, mwandishi raia wa Uganda, aliyehama nchi hiyo mapema miaka ya themanini, sasa amestaafu na anaishi Uganda.


Jarida la DW lilipofungwa mwishoni mwa miaka ya tisaini, aliandika makala katika gazeti la 'Monitor' jijini Kam-



Kwendo Opanga



Jaindi Kisero



Macharia Gaitho



Wachira Waruru



Lucy Oriang'



Mutegi Njau

pala akasema: "Chapisho la hadhi nchini Kenya limefungwa baada ya kuchapishwa kwa miaka 25, na kuwaacha baadhi ya waliojua historia yake wakihuzunika. Kwangu, hisia zangu zinazidi huzuni; zinakaribiana na majonzi yanayompata mtu aliyempoteza mpendwa wake."

Michael Ngwalla, alikuwa mweledi wa kuzungumza Kijerumani na aliwahi kuwa mwanamuziki jijini Vienna, Austria. Sasa anaishi Nairobi, akihudumu kama mwandishi wa kukodiwa.

Wahariri wa DW walikuwa: Kibe Kamuyu, aliyejiunga na 'Nation' ambako alipanda ngazi kuwa Mhariri wa Utayarishaji Nakala, kabla ya kustaafu, Janet Njoroge, mhariri msanifishaji, alijiunga na kampuni ya uchapishaji vitabu ya Longman Kenya Ltd, na kupanda ngazi hadi kileleni mwa kampuni hiyo, Wambui Githiora – Updike, aliyehamia Amerika na kuwa mwalimu wa shule ya upili na Wanjiru Ciira, ambaye pia amestaafu na anaishi Nairobi.

Wengine ni Lucy Oriang, aliyejiunga na gazeti la 'Daily Nation' na kupanda ngazi hadi kuwa Mhariri Msimamizi wa kwanza wa kike.

Betty Muriuki, ambaye pia alijiunga na NMG na kupanda cheo hadi kuwa Mhariri wa Makala kabla ya kujiunga na Wakfu wa Utafiti kuhusu Afya Afrika (AMREF).

Judith Ogecha alijiunga na 'Daily Nation' na kuwa Mhariri Msanifishaji na Joe Mugweru Mbuthia, aliyehudumu kama Mhariri wa Utayarishaji Nakala katika 'Daily Nation'. Alistaafu mwaka uliopita na anaishi Nairobi.

Wahariri wengine watajika, maripota na waandishi waliofanya kazi na DW ni: Nixon Kareithi, Margareta wa Gacheru, T J Mukui, John Mulla, Ben Omoro, William Ochieng', Blamuel Njururi, Profesa Calestous Juma, Mashet Masinjili, John Murumba, Chikati G. Bannaars, Joseph Makhoha, Nicholas Kamau, Tirop Simatei, Adalo Moga, Daniel Sifuna, Joe Rogoiyo, Tom Ochola and Rasna Warah.

Kurasa za jarida zilipambwa na picha zilizopigwa na Felix Obuna, Sam Ouma, Muturi Mwangi na William Kimaru.

Ilivyo kawaida ya maisha, kuna wanahabari wengi wa DW ambao walienda kuungana na wahenga. Miongoni mwao ni: Ben Omoro, Kuria Machang'i, Dishon Shangala, Muturi Mwangi, Mathew Gathigira, Dominic Odipo, na Amboka Adere.

# Ni jarida jipya: Jasiri changanuzi na sahihi



ALLAN **BULUKU**

*Ng''weno alipumua mara ya mwisho Julai 7, 2021 akiwa na umri wa miaka 83, lakini ndoto yake ingali hai. Kupitia kuzaliwa tena kwa mtoto wake, tumejitolea kudumisha wito wake kwa kukuletea uhondo ambao umeukosa kwa miongo miwili.*

Ni furaha yetu kuwakaribisha tena kwa jarida la 'Darubini ya Wiki' baada ya kulikosa kwa miaka 23.

Uchapishaji wa jarida hili ulipositishwa mnamo Mei 1999, huzuni uliwakumba wengi waliofahamu historia yake.

Kufufuliwa kwa mojawapo la majarida bora kuhusu habari za kisiasa, maoni na uchanganuzi barani Afrika kunaleta mwamko mpya katika taaluma ya uanahabari na demokrasia nchini Kenya.

Kwa miongo kadhaa, jarida hili lilikuwa kurunzi ya maisha yetu katika nyanja za jamii, siasa na maendeleo.

Waliopata nafasi ya kusoma 'Darubini ya Wiki' katika miaka ya sabini, themanini na tisaini wanaweza kuzungumzia mabadiliko katika siasa za Kenya kwa urahisi.

Hiyo ni kwa sababu jarida hilo la kila wiki liliwapakulia makala changanuzi kuhusu masuala ya siasa na uchumi kwa undani zaidi.

Maktaba kubwa na makavazi ya kitaifa yamehifadhi nakala zote za 'Darubini ya Wiki' ambazo zimeunganishwa vizuri ili wananchi, wenye haja ya kujua historia yetu waweze kuzisoma kwa urahisi.

Mmoja wa wahariri bora zaidi nchini, Hilary Ng'weno, alianza safari hii ya ujasiri baada ya Kenya kupata uhuru. Aliongozwa na msukumo wa kutumia nguvu za kalamu kuangazia mazuri na mabaya katika jamii yetu.

Alisomea katika Chuo Kikuu cha Harvard, Amerika -Mkenya wa kwanza kufanya hivyo, ambako alisoma Fizikia.

Hilary alihisi "kutengwa" na akakatiza masomo baada ya miaka miwili na akaamua kuhudhuria chuo kikuu katika uliokuwa Umoja wa Sovieti.

Lakini badala yake aliwasili Uingereza ambako alifanya kazi za sulubu kabla ya kurudi katika Chuo Kikuu cha Harvard kuendelea na masomo. Hatimaye alihitimu mnamo 1962.

Alizindua jarida hili mnamo 1975. Hilary aliongoza 'Darubini ya Wiki' katika mazingira ya kisiasa yenye changamoto nyingi ambapo uhuru wa wanahabari ulidhibitiwa na demokrasia ilikuwa jambo geni.

Kama mwanahabari jasiri, alisimama kidete na kuchapisha makala ya kisiasa yaliyochochea hisia za wasomaji na maoni ambayo mara nyingi yalikera serikali, ambayo mamlaka yake yalikita kwa mtu mmoja - Rais.

Ng'weno aliaga dunia Julai 7, 2021, akiwa na umri miaka 83, lakini ndoto yake ingalipo.

Tungependa kuweka wazi kwamba: Kama chapisho, hatuegemei itikadi yoyote ya kisiasa; tumeweka viwango ambavyo vitahakikisha kwamba tunapakua yale ambayo yatawafaa watu wote.

Jarida hili litashughulikia mahitaji ya Wakenya wote - bila kuzingatia imani, rangi, kabila, umri, jinsia au mirengo ya kisiasa.

Ni matumaini yetu kwamba, kupitia jarida hili lililozinduliwa upya, kila msomaji atapata nafasi ya kuwasilisha maoni, imani na tajriba yake. Hii ndiyo maana tuko hapa.

Kwa misingi ya historia nzuri ya jarida la 'Darubini ya Wiki', tutaendesha shughuli zetu kwa njia ya uwazi kadiri tuwezavyo.

Umealikwa kuwasilisha makala kwa ajili ya kuchapishwa, ambayo yatakaguliwa kwa kuzingatia viwango vyetu vya uhariri.

Makala ambayo yatapita mtihani huu yatachapishwa katika jarida hili tunaloamini litaleta mwamko mpya katika taaluma ya uanahabari Kenya.

Ni furaha yetu kwamba tunaendeleza malengo ya jarida la 'Darubini ya Wiki' huku tukipata kauli zenu.

Tuna hamu kuwa ya kuwa sehemu ya historia hii. Twende kazi.

*abuluku@ke.nationmedia.com*

# Habari kwa picha



Mwanachama wa kundi la Saraya al-Salam (Kikosi cha Amani), jeshi linalohusishwa na kundi la kidini la Shiite, Moqtada al-Sadr, akimsaidia mwanamke kufyatua bunduki wakati wa makabiliano na wanajeshi wa Iraq, katika eneo la Green Zone, mjini Baghdad, Agosti 30. PICHA |AFP



Samuel Oliech (katika) akibeba mpira na kumpiga chenga Femi Sofolarin wa Scotland wakati wa mechi ya mashindano ya Los Angeles 2022 World Sevens Series, uwanja Dignity Health Sports Park, mjini Carson, California Agosti 27. PICHA |AFP



Serena Williams akisherehekea baada ya kumshinda Danka Kovinic wa Montenegro wakati wa raundi ya kwanza ya mechi yao ya 2022 US Open katika uwanja wa USTA Billie Jean King National Tennis Center, mjini New York, Agosti 29. PICHA |AFP



Mwanaume akiendesha mkokoteni wa punda Agosti 30, wakti wa mvua kubwa mjini Dera Allah Yar, eneo la Jaffarabad, jimbo la Balochistan, mbalo limekumbwa na mafuriko makubwa. PICHA |AFP




Watu wakisafiri kwa trekta wakitoroka mafurika nyumbani kwao kutokana na mvua kubwa katika eneo la Shikarpur, Pakistan, Agosti 30. PICHA |AFP



Jumba liliporomoka eneo la Mariupol, kutokana na uvamizi wa jeshi la Urusi nchini Ukraine Agosti 28. PICHA |AFP



Mwanamitindo akionyesha mavazi kutoka UCF 2023 S/S Collection wakati wa hafla ya Tokyo Fashion Week, mjini Tokyo, Agosti 30. PHOTO |AFP



# KINYOZI ZAIDI YA WENGINE

*Stephen Ndegwa si mwanasiasa wa kawaida. Baada ya kulelewa katika familia pungufu, alipigana na unyonge na kutumia kipaji chake cha kunyoa kushinda udiwani Kaunti ya Nairobi.*

NAFASI YA VIJANA

# MAISHA KAMILI

**SAUTI YA VIJANA** Utagundua dhana yako kuwahusu ni potovu punde tu ukikutana na baadhi yao waliofaulu kiuchumi kushinda wenzao walio na umri mkubwa.

● NA MOSES OJWANG



Mtazamo maarufu wa vijana Wakenya katika fikra za wengi ni vijana wa kiume na wa kike wanaoishi katika nyumba za wazazi wao; wakiitisha chakula na mavazi hadi wanapohitimu miaka ya thelathini; mapozi ya kizazi kilichopotea kinachotafuna 'muguka' chini ya miti na kwenye vioski huku wakichati kwenye simu zao na kutazama vichekesho vya 'Tik Tok'.

Hawa ni vijana ambao hawajaajiriwa, wasio na lolote linalowasumbua. Huu ni mtazamo usio wa kweli na dhana hiyo hutoweka haraka unapokutana na vijana waliomakinika na kufanikiwa zaidi kiuchumi kushinda wenzao waliowazidi umri.

Mjini Mombasa, nilikutana na vijana saba wa kiume wenye umri usiozidi miaka 20. Kazi yao imepangwa vyema na hakuna anayejua walikojifunzia kazi. Walifaulu wenyewe bila usaidizi kutoka popote; motisha na ari yao binafsi tu.

Sasa wana maduka matatu ambayo wameyageuza kuwa gereji ndogo. Barobaro hawa waliwahi kuwa waendeshaji boda boda lakini wakaona ubwege wa kutumia muda mwingi wakitegea kiasi kidogo cha pesa na kisha kuzitumia zote kwa siku moja.

Waligundua kuwa vijana wengi zaidi wasio na mawazo ya kujiendeleza kibinafsi wanazidi kuongezeka katika biashara ya usafirishaji wa pikipiki na hapo ndipo wazo liliwajia. Baada ya miaka miwili ya kuendesha pikipiki zao zilizowapa faida ndogo, walianza kuzikusanya na kuziunda mpya.

Idadi kubwa, kama si wafanyabiashara wote wanaoagiza pikipiki nchini, huwa hawaleti pikipiki nzima. Kila sehemu huja kivyake hivyo basi mwagizaji ni sharti aziunganishe ili kuunda pikipiki nzima. Kwa njia hii, shehena moja inaweza kubeba vijisehemu vingi ambavyo kwa kawaida huchukua nafasi ndogo kushinda pikipiki nzima.

Vijana hawa walianza kuwaendea waagizaji sehemu hizo nchini na kuwaomba kazi ya kuwanganishia pikipiki kwa malipo.

Walianza kazi hiyo chini ya mti mkubwa ambapo waliunda pikipiki sita hadi nane kwa siku.

Waliweka akiba ya mapato yao, na katika kipindi cha miezi sita kamili, biashara yao iliimarika na walikuwa wakitafutwa sana kwa kazi yao nzuri.

### Kampuni za magari

Wazo la kwanza linalokujia ukikutana nao ni kwamba huwa tu wanafanya kazi na kugawana pesa baina yao mwishoni mwa siku.

Lakini umenoa! Hawa ni wataalamu, matumizi ya peza zao yamepangwa sawasawa; huwa wanalipa ushuru kuambatana na sheria na pia wanajilipa mishahara ya kila mwezi unapokamilika.

Kazi yao imekuwa rahisi zaidi siku hizi sawa na katika nyanja ya uundaji wa bidhaa kwa wingi katika kampuni kubwa za magari kama vile Ford na Toyota, kila mtu binafsi akishughulikia sehemu mbili au tatu katika uundaji wa pikipiki; ni jambo la kuvutia sana kuona pikipiki ikijitokeza huku ukitazama kwa mshangao.

Kazi yao hii inamfanya mtu kufikiria kuwa kuna kazi ya kufanya hapa nchini, kinachokosekana ni ajira rasmi tu.

*Je, wewe ni kijana na una ari ya kufanikiwa? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni na mtazamo wako kuhusu masuala ibuka kupitia: weeklyreview@ke.nationmedia.com*

## KAULI YANGU



**Seraphine Okeyo**
Vijana wamekuwa kitengo mashuhuri nchini. Hii inasisitiza umuhimu wa kushiriki katika chaguzi kwa sababu kunawapa fursa ya kuwa na sauti kuhusu viongozi wao wapya. Vijana wana mahitaji maalumu.
*— Miss Heritage Kenya*



**Wangu Kanuri**
Chaguzi zilizokamilika majuzi zinaonyesha mamlaka ni ya vijana. Wanaweza wakaamua mustakabali wa taifa hili. Ikizingatgiwa idadi kubwa ya watu ni vijana, wengi wao walichaguliwa afisini mnamo Agosti 9. Naamini watahusika katika kufanya maamuzi.
*— Mwanahabari*



**Belly Kanaitsa**
Vijana wengi walishinda nyadhifa mbalimbali. Vijana pia walijifunza athari ya uenezaji wa habari za uongo na potovu kwenye mitandao ya kijamii; athari ya habari feki na matini yenye madhara mitandaoni. Tujifunze kila wakati kuwa waadilifu.
*— Mtaalam wa mikakati kidijitali*



**Alex Khamoyi**
Chaguzi huwapa Wakenya fursa ya kuamua mwelekeo wa taifa. Vijana, walio wengi, walikuwa na fursa ya kuchagua viongozi ambao watatetea maslahi yao na hilo ndilo jambo muhimu. Mambo yatakuwa bora zaidi 2027.
*— Mfanyabiashara*

KAULI YANGU



# HALI MPYA YA KAWAIDA

**ULIMWENGU BAADA YA JANGA:** Kampuni nyingi zilibadilisha mfumo wa kazi kuwa wa mtandao na zikafaulu katika kipindi cha janga la Covid-19. Hatua hiyo iliziwezesha kupanua ofisi zao.

Mnamo Desemba, 2019 nilifanya mkutano na mteja mmoja anayehudumu katika sekta ya utengenezaji bidhaa. Alizungumza kuhusu tukio fulani nchini China ambalo halikueleweka wazi wakati huo, ingawa alibashiri lingechangia kusitishwa kwa shughuli duniani.

Shughuli za mteja huyo hutegemea sana malighafi kutoka ng'ambo lakini baada ya wiki chache hakuweza kusafirisha bidhaa kutoka China kuzileta Kenya. Ni wakati huo ambapo nilianza kufuatilia kwa makini ugonjwa wa Covid-19.

Baadaye Machi 2020 kisa cha kwanza cha maambukizi ya ugonjwa huo kiliripotiwa nchini na serikali ikatangaza masharti kadhaa yaliyolenga kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo. Matokeo yake ni kwamba wengi wetu tulilazimika kufanya kazi kutoka nyumbani.

Kwa njia nyingi, janga la Covid-19 limeathiri nyanja mbalimbali za maisha ya wanadamu. Ingawa madhara mengine kama vile vifo, kupotea kwa nafasi za ajira na kudorora kwa uchumi yaliumiza zaidi, janga hilo pia lilileta mazuri.

Kwa mfano, tulibuni mtindo wa kufanya kazi kutoka nyumbani, jambo ambalo hatukutafakari kuhusu kabla ya ujio wa ugonjwa huo.

Mtindo huo wa kufanya kazi umewafaa baadhi ya wafanyakazi na waajiri zaidi kuliko ule wa kawaida wa kufanya kazi afisini kati ya saa mbili za asubuhi hadi saa kumi na moja jioni.

Wafanyakazi na wakubwa wao wamekuwa wakishauriana kwa urahisi kwa simu na mitandao ya kijamii kwa saa 24 kila siku.

Haya yote yalifikiwa bila gharama zinahusiana na mtindo wa kufanya kazi ofisini kama vile ulipaji kodi, intaneti, vifaa vya matumizi ya kimsingi, utunzaji vifaa na ada za huduma nyingine za kufanikisha kazi.

Mtindo wa kufanya mikutano kwenye majukwaa ya dijitali kama Zoom, Google, Hangout, Microsoft Teams na hata mtandao wa WhatsApp umepanua mawanda ya afisi hadi nje ya nchi.

Tuliweza kutekeleza miradi kwa ukamilifu kupitia kwa mitandao hadi kufikia mataifa ya Ethiopia, Misri, Tanzania, Nigeria na Zambia, yote ikiwezeshwa na matumizi ya teknolojia.

### Uandalizi wa shughuli mbalimbali

Aidha, tulibuni upya namna ya kuendesha shughuli mbalimbali kuambatana na mabadiliko ya haraka ulimwenguni.

Ingawa shughuli nyingi zilifutiliwa mbali ili kutimiza masharti ya kuzuia kusambaa kwa Covid-19, hii haikuchukua muda mrefu kwa sababu maisha yalifaa kuendelea.

Kama mtaalamu wa uhusiano mwema na mwandalizi wa hafla mbalimbali, tulipunguza idadi ya watu waliohitajika kuhudhuria au tuliendesha mikutano katika mitandao.

Vile vile, tuliandaa mikutano inayotumia mfumo wa ana kwa ana na ule wa mtandaoni.

Hii iliwezesha kila mtu kuhisi kushirikishwa moja kwa moja.

Ingawa janga la Covid-19 lilibadilisha mbinu na mfumo wa maandalizi ya hafla, waandalizi walifaidika pakubwa badala ya kazi zao kutishiwa.

Kumekuwa na madai kuwa kampuni nyingi zinapendelea watu wenye ujuzi wa kuandaa hafla kupitia mitandao ya kijamii badala ya maafisa wa uhusiano mwema, kama ilivyokuwa hapo awali. Ukweli ni kwamba madai haya ni ya uongo.

Kwa hakika kampuni, biashara mbalimbali na asasi za serikali zinaendeshwa kwa misingi ya malengo maalumu ambayo yanaweza tu kufikiwa kupitia mikakati ya mawasiliano inayojumuisha mbinu na mifumo yote ya mawasiliano.

Kimsingi, mikakati hiyo hutayarishwa na wataalamu katika nyanja ya mawasiliano, ambao hushirikisha wajuzi katika mawanda ya mitandao ya kijamii, kabla ya kuwasilisha mapendekezo kwa wateja wao.

Kwa njia hii, nyanja hizi mbili za mawasiliano hazishindani bali zinasaidiana katika kufanikisha malengo sawa.

Huku maambukizi ya Covid-19 yakiendelea kupungua, ni muhimu kutaja kuwa changamoto peke iliyoletwa na mtindo wa kufanyia kazi nyumbani ni ugumu wa kutoa mafunzo ya ziada kwa wafanyakazi.

Imekuwa vigumu kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa njia bora, hasa kwa walio na umri mdogo.

Matokeo yake ni kwamba kampuni nyingi, ikiwemo yetu, imerejelea mtindo wa kufanya kazi ofisini.

Hata hivyo, majukumu ambayo yanaweza kutekelezwa kupitia mitandao bado yanakubalika.

Kadiri muda unavyosonga, uendeshaji wa kazi ya uhusiano mwema kidijitali umekuwa sehemu ya mikakati yetu ya kuwahudumia wateja wetu.

Kwa kuendesha shughuli nyingi kupitia mitandao, tumeweza kuvumisha biashara yetu na kuvutia wateja wengi.

Kevin Otiende ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Uhusiano Mwema kwa jina, CALLA PR

*kevinotiende1@gmail.com*

SUALA KUU

# KINYOZI SASA NI DIWANI

**BIDII ILIYOKIUKA MIPAKA:** Stephen Ndengwa alitumia ushirikiano mwema na watu na ujuzi wa kunyoa kushinda kiti cha Bunge la Kaunti la Nairobi

● NA AMINA WAKO

MAISHA wakati mwingine ni siri ambayo mwelekeo wake haufahamiki na wengi. Bw Stephen Ndegwa, Mwakilishi Mteule wa Wadi ya Parklands/Highridge, Nairobi, ni miongoni mwa watu wanaofahamu kikamilifu uhalisia huo.

'Darubini ya Wiki' ilipokutana naye Jumatatu asubuhi wiki iliyopita, Ndegwa alikuwa akiendelea na shughuli za kawaida katika duka lake la kinyozi, Fine Cuts, katika eneo la Westlands, Nairobi.

Alitupa nafasi kumhoji huku akiendelea kumhudumia mteja wake. Tulipoketi chini kuanza mahojiano, simu yake ilikuwa ikilia kila mara. "Ninafaa kukutana na wahudumu wa bodaboda ambao wamehamishwa kwa nguvu kutoka eneo wanakowabebea abiria wao," akasema.

Ndegwa alizaliwa na kulelewa katika mtaa duni wa Kangemi, alikofanya kila awezalo kukabiliana na ugumu wa maisha kila siku.

Mama yake alikuwa akiuza pombe ya 'Chang'aa' kupata pesa za kumlea Ndegwa na ndugu zake. Aliingilia biashara hiyo baada ya mumewe kumuacha na kuoa mwanamke mwingine. "Niliteseka sana nikisoma kwa sababu biashara ya chang'aa haikuleta mapato ya kutosha kukidhi mahitaji ya familia yetu. Mara nyingi, mama yangu alikamatwa na polisi kwa kuendesha biashara hiyo haramu na kutuacha peke yetu," akaeleza.

Ingawa maisha yalikuwa magumu, alifanikiwa kumaliza shule ya upili na mama yake akajikakamua kumpeleka katika taasisi ya mafunzo ya kompyuta jijini.

Hata hivyo, Ndegwa alikuwa na maono tofauti: alitamani kuwa dereva wa basi. Ni ndoto iliyochochewa na hadithi ya Bw Kamau kwenye kitabu cha 'Hallo Children', kilichosomwa na wanafunzi wa shule ya msingi katika miaka ya themanini na tisini.

Kozi ya kompyuta iligeuka kuwa ghali sana kwa mama yake kumudu kulipia. Aliachana nayo.

**Shabaha yangu ni kubadilisha maisha ya jamii kwa kuzidisha ushirikiano katika mipango, kuhakikisha wakazi wanapata huduma bora za matibabu na msaada wa masomo, na kukuza vipaji na miradi ya maendeleo ya biashara kwa vijana.**



Shangazi yake mmoja alimshauri mama yake ampeleke kwa kozi ya kinyozi jijini. Ndegwa alikubali wazo hilo ingawa alikuwa na matamanio mengine.

Kwa bahati nzuri, alipata kazi ya muda kama manamba wa matatu. "Baada ya masomo kila siku, nilifanya kazi ya muda kama manamba. Nilikuwa na imani kuwa baadaye ningefanikiwa kuwa dereva," akaeleza.

Kazi ya umanamba aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi John Michuki alipoweka sheria kali kulainisha sekta ya matatu. Ndegwa aliamua kuendelea na masomo ya kinyozi. Alipata kazi ya kinyozi katika duka moja eneo la Westlands.

"Baada ya kumaliza kozi na kujitosa katika sekta ya kinyozi, sikuamini kuhusu ningeweza kunyoa watu wa hadhi waliokuwa wakifika katika duka hilo," akaeleza.

Baada ya muda, baadhi ya wateja wake walianza kuwekwa magazetini kama wanamitindo. Hapo ndipo alipata imani na nguvu ya kuzamia kikamilifu taaluma hiyo.

Alikusanya pesa na kuanzisha duka lake mwenyewe, ambapo alikuwa akiwatoza wateja wake Sh30.

Miaka 12 baadaye, Ndegwa anakubali kuwa si rahisi kuendesha biashara. Anawashukuru wateja wake kwa kumwezesha kutembea naye katika safari hiyo.

"Nilikuwa na ujuzi wa kunyoa lakini sikuwa na ujuzi wa kuendesha biashara. Biashara inahitaji ujuzi wa kipekee," akasema.

Tamanio la Ndegwa kuwa mwanasiasa lilitokana na utangamano wake na wanasiasa maarufu akiwemo aliyekuwa Waziri Mkuu, Raila Odinga, ambaye alikuwa miongoni mwa wateja wake.



**Mwakilishi mpya wa Wadi ya Parklands/Highridge, Stephen G. Ndegwa, katika duka lake ya kinyozi, la Fine Cuts Spa, Westlands, Nairobi.**
FRANCIS NDERITU I NATION

Mnamo 2013, alitangaza nia ya kuwania nafasi ya Mwakilishi Wadi eneo hilo la Parklands/Highridge. Lakini hakutimiza ndoto yake kwa kukosa pesa.

Ikizingatiwa biashara yake haikuwa ikifanya vizuri, aliahirisha mpango huo hadi 2017 akitarajia angepata pesa za kutosha kufadhili kampeni zake.

Aliamua kupanua biashara yake kwa kuanzisha taasisi ya mafunzo ya urembo. Hata hivyo, alihitaji mkopo.

Aliacha kulipia kodi duka lake kuu ili kuongeza pesa ambazo

zingemwezesha kupewa mkopo na benki. Alikuwa amepanga kuendesha mpango huo kwa miezi minne.

Lakini mwenye nyumba hakungoja. Alipiga mnada vifaa vyake ili kupata kodi ambayo hakuwa amelipa. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa changamoto zake za pesa.

Mwaka huo huo, maduka yake mengine yaliharibiwa kwenye shughuli ya ubomoaji iliyokuwa ikiendelea katika Soko la Westlands. Kutokana na changamoto hizo, mwanawe alipoteza nafasi ya kujiunga na Shule ya Upili ya Wasichana ya Alliance, baada ya kufanya vizuri sana katika mtihani wa Darasa la Nane (KCPE).

"Hali ilikuwa mbaya sana. Nilitamani kufa. Niliogopa kurudi nyumbani siku hiyo kwani sikujua nitamwambia mwanangu," akaeleza.

Kupitia usaidizi aliopata kutoka kwa wateja na marafiki wake,

aliamua kujitosa tena kwenye ulingo wa siasa kwenye uchaguzi mkuu

wa 2022. Alijipata katika hali ngumu tena



baada ya mrengo wa Azimio – One Kenya kuweka mkakati ambapo ni vyama fulani tu vya kisiasa vingeruhusiwa kuwania nafasi tofauti katika maeneo fulani.

"Nilikirai chama changu, ODM, kufanya utafiti kubaini kiwango cha umaarufu wa kila mgombeaji kabla ya kufanya maamuzi. Baada ya hilo, vyama vyote vilivyo katika muungano huo viliruhusiwa kusimamisha wagombeaji wake," akasema Ndegwa.

Ndegwa, ambaye ni baba ya watoto watatu, anasema siasa za Kenya zinahitaji mtu kuwa tayari kuhimili mawimbi ya kisiasa. Anasema alishambuliwa mara tatu na kujeruhiwa vibaya. Mkewe aliogopa sana kiasi cha kumwambia ajiondoe kwenye kinyang'anyiro hicho.

"Tulikosana kuhusu kampeni zangu kwa sababu alikasirishwa na niliyokuwa nikifanya. Kila mara, alionekana kuwa mwenye mawazo kutokana na niliyokuwa nikipitia," akasema.

Anaeleza kuwa kampeni yake ilifadhiliwa na Wasamaria Wema. "Nilipata msaada mkubwa kutoka kwa marafiki wangu katika Soko la Westlands. Baadhi ya watu waliamua kutengeneza mavazi ya kampeni huku wengine wakinitengenezea mabango," akaongeza.

Nilifanya kampeni zangu kutoka nyumba hadi nyingine. "Ikizingatiwa kuwa nimefanya kazi hapa kwa zaidi ya miaka 12, ninafahamu changamoto zinazowakabili wafanyanyabiashara. Lengo langu kuu ni kubadilisha maisha ya wenyeji, kwa kuwahusisha kwenye mipango ya

maendeleo, kuboresha huduma za afya na elimu na kuhakikisha vijana wanapata nafasi nzuri kuendeleza vipaji vyao," akasema.

Wakati wa kampeni, Ndegwa angeenda kwenye duka lake

mapema sana na nyakati za jioni ili kupata pesa za kukidhi mahitaji ya familia yake.

Mwanawe, anayesoma katika Shule ya Upili ya Wasichana ya Mugoiri, atafanya Mtihani wa Kidato cha Nne (KCSE) mwaka huu. Licha ya kuchaguliwa Mwakilishi Wadi, Ndegwa anasema bado ataendelea na shughuli za kawaida katika duka lake.

"Nataka kupanua biashara hii na kuajiri watu zaidi ya wanane nilio nao kwa sasa. Bado nina mpango wa kubuni taasisi ya mafunzo, ambapo vijana watapata nafasi kujifunza masuala ya urembeshaji na usimamizi wa biashara," akaeleza.

Anasema licha ya nafasi yake mpya, atakuwa tayari kuwanyoa wateja wake.

LAMU YATAMBULIWA

# MFALME WA FILAMU

**MMOJA WA WATENGENEZAJI FILAMU BORA NCHINI:** Mtengenezaji filamu chipukizi anabadilisha maisha ya vijana kwa filamu zake ambazo zimemshindia tuzo

Ametumia taaluma yake inayostawi kuunda nafasi za kazi na kuwapa motisha vijana mjini Lamu. Akiwa na umri wa miaka 28 pekee, Daudi Otieno Anguka ni nguzo ya matumaini katika kisiwa hiki, ambacho amekigeuza kuwa eneo mashuhuri kwa baadhi ya sinema za runinga zinazotazamwa zaidi Kenya.

"Wakati utakuwa ukipigania kiti kwenye meza, nitakuwa Lamu nikiunda changu," akasema katika mahojiano.

Mzaliwa wa Mombasa, kazi za produsa huyu mtajika zinajumuisha kipindi cha televisheni kwa jina 'Pete', ambacho ni sinema maarufu ya Kiswahili iliyopeperushwa kwenye kituo cha MultiChoice cha Maisha Magic East kwa vipindi vitano.

Tajiriba ya kuunda filamu ya 'Pete' ilifungua pwani ya Kenya kwa ulimwengu wenye fursa chungu nzima katika sekta ya sinema.

"Tulirekodi filamu hiyo katika Kisiwa cha Funzi tukiwa na kikosi cha waunda sinema 70. Ilikuwa kazi kubwa sana ambayo kisiwa hicho kidogo kimewahi kushuhudia," anasimulia.

Alipokuwa mdogo, mama yake Anguka alitaka awe mhandisi lakini moyo wake ulikuwa katika uundaji wa filamu. Anguka, ambaye ni mtoto wa pili katika familia ya watu tisa, alisomea Shule ya Msingi ya Unicef Academy na Shule ya Upili ya Kajembe. Mjini Mombasa.

Alikamilisha elimu yake ya sekondari mnamo 2011, lakini wazazi wake hawakuwa na hpesa za kumpeleka chuo kikuu. Aliungana na mama yake kuchuuza mandazi na samosa eneo la Mikindani ili kujikimu kimaisha. "Nilipokuwa shule ya msingi, nilipenda kutazama sinema za vipindi na nyimbo ambazo zilichochea ari yangu katika filamu. Nilijiunga na klabu cha uigizaji katika shule ya sekondari na hapo ndipo uraibu wangu wa kuigiza ulipoanzia," anaeleza.

Baada ya kuchuuza chakula kwa miaka miwili, Anguka alikuwa amekusanya hela za kutosha kumwezesha kujiunga na Shule ya Filamu ya Hot Sun, Nairobi, ambapo alisomea uundaji wa filamu na kufuzu 2016. Alianza kwa kuundia Maisha Magic filamu fupi ambayo haikuwa na bajeti. "Niliwashawishi kuwa ninaweza kufanya hivyo na tukatia saini mkataba. Hapo ndipo ufanisi wangu ulipoanzia," anasema.



Anguka anahisi kuwa mwenye bahati kufanikisha ndoto yake ya utotoni. Lakini kinachomridhisha zaidi ni kwamba anaweza kabadilisha maisha ya watu kwa kukuza vipaji vichanga katika ulingo wa filamu na kuunda ajira.

"Nina watu wanaonitegemea. Katika eneo moja, tunaweza kushirikisha watu wa ziada wapatao 300. Wote huwa wanalipwa. Ninapoenda nyumbani, hata nikiwa nimechoka namna gani, ninajua moyoni mwangu nimechangia upande wangu kuboresha jamii."

Anataja msimu wa Covid-19 kuwa kipindi kilichokuwa kigumu zaidi katika taaluma yake.

"Nilikuwa na watu 120 wakifanya kazi na kulipwa mshahara kamili. Kila kitu kilipofungwa mnamo 2020, singeweza kumudu kuwalipa. Walikuwa wakinipigia simu, wakinisihi niwape pesa za kulisha familia zao. Kwa miezi kadhaa suala hili lilinіathiri sana. Nilitangaza shida yangu hiyo kwa kampuni ya MultiChoice na kwa bahati nzuri wakanielewa na kuniokoa.

Mwanakamera Hamisi Omar anasema ni baraka kubwa kufanya kazi na Anguka. "Amefanyia kazi miradi mikuu. Nilipokutana naye, alinihimiza nifanye bidii na kutoa kazi bora kwa kila kitu nilichorekodi kwa kamera. Ni kiongozi shupavu kazini na sifa hiyo ndiyo imetufanya kuendelea kusonga mbele."

Sharif Mohammed Kero, ambaye ni mkurugenzi wa uundaji filamu, aliajiriwa mara ya kwanza kuelekeza kipindi cha 'Sanura'. "Tulikuwa tukikaa bure tu bila cha kufanya lakini sasa biashara




**Mtengenezaji filamu na mwelekezi Daudi Otieno Anguka wakati wa kutegeneza filamu ya 'Sanura', Kauti ya Lamu.**

ni nzuri. Kuna nafasi nyingi. Nimeajiriwa kwa miaka sita, jambo ambalo halijawahi kutokea maishani mwangu."

Licha ya ufanisi wake, Anguka anataja mfumo wa Kenya unaotoza kiasi cha juu mno cha ushuru kama kizuizi kikuu kinacholemaza ukuaji wa sekta hiyo.

"Kuunda filamu nchini Kenya si rahisi. Tunateseka kwa sababu ya kodi nyingi zinazotozwa na wasimamizi. Badala yake, serikali inafaa kutoa ufadhili ili kupiga jeki na kupigia debe eneo la pwani kama kituo cha utalii wa filamu," anapendekeza.

Anguka ameshinda tuzo kadhaa ikiwemo Filamu Bora (Afrika Mashariki) Sinema Bora ya Lugha ya Kwanza na Tuzo la Vipindi katika Uteuzi wa Watazamaji wa Africa Magic 2017 kupitia filamu yake, 'Zilizala'. "Tuzo hizo zilinihimiza kujitahidi zaidi katika uundaji wa filamu za vipindi vya televisheni," anasema.

"Nilikuja Lamu kwa sababu ya mazingira yake ya kipekee. Nilipokuwa nikisaka maeneo mwafaka katika visiwa vyake saba, niliangazia kinachoendelea katika jamii ya kisasa na nikatumia mawazo kutoka kwa watu mbalimbali kubuni hadithi ya 'Sanura'," anaeleza.

"Kipindi hicho kinasawiri utamaduni wa Waswahili ikiwemo mavazi, vyakula, mziki, itikadi na tamaduni ambazo zimehakikisha Lamu imedumisha sifa zake za kipekee ambazo zimekuwa sehemu yake kwa miaka 700 iliyopita."

Anasema "hadithi hiyo inasawiri wahusika wa kubuni na mtiririko wa matukio lakini kuunda kazi hiyo katika mazingira ya kwetu pia kulitupa fursa ya kuchochea mazungumzo kuhusu viambajengo vya utamaduni wetu ambavyo huenda vingepitwa na wakati. Televisheni ni ulingo mwafaka ya kuwasilisha mvutano kati ya wasiwasi wa kizazi cha wazee wanaohofia kuachilia utamaduni na ukosefu wa subira kwa wataalamu wachanga wanaotaka kuacha itikadi zilizopitwa na wakati."




Hii ndiyo kazi ya kwanza ya aina hii katika eneo hili; hatua ya kujitolea kwa MultiChoice kuwekeza kiasi hiki inatarajiwa kuvutia waundaji filamu wengine kutoka humu nchini na kimataifa katika eneo la pwani.

Hususan Lamu, inayosheheni majengo yenye kiwango cha juu cha Uswahili, manukato yanayohanikiza historia nzito katika kila pembe na minara ya jadi ya kuvutia iliyojengwa kwa miundo ya Kireno na kupangwa mitaani, ni tunu adimu kwa kamera yoyote.

Kulingana na Unesco, sekta ya filamu na televisheni inayozidi kunawiri nchini huenda ikawa mbinu ya kuvutia mapato ya kigeni huku taifa likiuza talanta na vifaa kwa mataifa ya kigeni.

Tayari Anguka ananufaika kutokana na kituo hiki kwa kuangazia Lamu, ambayo hadi sasa ni moja kati ya siri za Bahari Hindi zilizohifadhiwa vyema zaidi.

## tahariri




■ Adhabu kali itangazwe ili kuwa onyo wanaolaghai Wakenya haki yao ya kupiga kura

# Wanaohujumu uamuzi wa wananchi



KWENDO
OPANGA

Siku sitini zilizopita, wakiwa na matumaini na huku wakidumisha amani Wakenya alijitokeza kushiriki Uchaguzi Mkuu. Walipiga kura kuwachagua viongozi watakaowawakilisha kama madiwani, Wabunge, Maseneta, Wabunge Wawakilishi wa Kaunti, Magavana na Rais.Lakini kwa sababu Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), inayoongozwa na Bw Wafula Chebukati imegawanyika Wakenya bado hawajui waliyemchagua kuwa rais wao mpya.

Hii ndio maana wataelekeza macho yao na kutega masikio yao kwa Mahakama ya Juu kesho majaji wake saba watakapoamu ikiwa Naibu Rais William Ruto alitangazwa kwa njia halali na Chebukati kuwa Rais mteule mnamo Agosti 15 au laLakini hata ingawa mahakama hiyo, inayoongozwa na Jaji Mkuu Martha Koome ikiamua kwamba Ruto hakutangazwa mshindi kisheria, huenda Wakenya wasijue walichosema, na jinsi walivyoisema, mnamo Agosti 9.

Na bila kuzingatia uamuzi ambao mahakama hiyo itatoa, Kenya watasalia wakiwa wamegawanyika kwa muda.Hii ndio maana Jaji Koome na wenzake wanahimizwa kuzingatia kuwa nchi hii sharti iwepo baada ya wao kutoa uamuzi wao. Kutokea kwa migawanyiko nchini kwa sababu ya uchaguzi sio jambo geni lakini uchaguzi usiosimamiwa vizuri husababisha migawanyiko hata zaidi.Hata hivyo, mahakama haina mamlaka ya kuwaambia Wakenya ni nani alishinda katika uchaguzi mkuu wa Agosti 9.Wakati huu, mambo ambayo yanajulikana wazi wazi kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Agosti 9 na haswa uchaguzi wa urais, ni foleni ndefu za Wakenya wakisubiri kupiga kura na bajeti ya kubwa ya Sh44.6 bilioni ya kufadhili shughuli hiyo.

**Majaji na kundi la mawakili kazi ya kuhesabu, kutathmini na kutuma matokeo kwa mikono na kwa njia ya kielektroniki, hasa ya urais, imekuwa shida kubwa ya kila mara kwa IEBC.**

Hata hivyo, uhalisia huu unavurugwa njama iliyopangwa kuvuruga matokeo ya uchaguzi wa urais.Hii ndio maana majaji wameulizwa, kwa mara ya tatu katika mihula mingi ya uchaguzi, kubaini uamuzi ambao Wakenya walifikia debeni kuhusu ni nani walitaka awe Rais wa tano wa taifa hili.Lakini shida ni kwamba Mahakama ya Juu itaelekezewa lawama kuhusu namna ambavyo itaamua.Hii ni baada yake kupoteza katika kesi aliyowasilisha kupinga ushindi wa Rais Uhuru Kenyatta.Mnamo 2017, IEBC ilitangaza kuwa Bw Odinga alishindwa katika uchaguzi wa urais, lakini Mahakama ya Juu ilibatilisha ushindi wa Rais Kenyatta na kuamuru uchaguzi mpya ufanyike.Rais Kenyatta aliyepandwa na hasira kufuatia uamuzi huo aliwarejelea majaji wa mahakama hiyo kama "wakora" walionyakua ushindi wake na kuahidi kuwaadhibu.Alifoka kwamba majaji hao sita hawakuwa na haki ya kubatilisha uamuzi wa mamilioni ya wapiga kura.Bw Odinga alisherehekea uamuzi huo kwa muda kabla ya kususia marudio ya uchaguzi kwa sababu, kwa mtazamo wake, IEBC ingeiba kura zake tena.


Hata hivyo, IEBC iliendeleoa na uchaguzi uliooshirikisha Rais Kenyatta na kiongozi wa Chama cha Thirdway Alliance Ekuru Aukot.Rais Kenyatta aliibuka mshindi na kuapishwa kuanza muhula wake wa pili na wa mwisho. Muhula huo uliopaswa kukamilika baada ya ushindi wa uchaguzi wa urais kubainika waziwazi baada ya uchaguzi wa Agosti 9.

Mahakama hiyo sharti itoe adhabu kali kwa wahusika katika maovu hayo ili kuzuia kutokea kwa vitendo hivyo vya kuwapokonya haki yao ya kujichagulia raia wao.Pili, kwa kufahamu kuwa IEBC imewahi kusimamia vibaya chaguzi mbili mtawali, Koome na wenzake, wasiiruhusu kusimamia uchaguzi mwingine.Endapo tume hii ingeadhibiwa mnamo 2017 kwa makosa iliyotenda, Kenya haingejipata katika hali ya sasa.Tatu, kwa sababu watu wengi watalalamika ikiwa majaji watageuka wanaharakati, kando na kutunga sheria zao, wanapaswa kupendekeza kuwa bunge litunge sheria itakayotoa hakikisho la kufanyika kwa uchaguzi huru, wenye haki na ambayo matakeo yake yataaminika.

maoni

■ Kumekuwa na msururu wa wahariri stadi wakisukuma gurudumu la uanahabari

# HBN: Mhariri stadi, mcheshi na aliyetambua vipaji kwa urahisi



MACHARIA GAITHO

KAMA Hilary Ng'weno hakuwa na sifa ya ucheshi na uwezo wa kutambua vipaji mapema, wengi wetu hatungekuwa wanahabari.

Alikuwa mtu roho safi aliyewapa nafasi watu ambao hawakuwa wamesomea uanahabari kujaribu vipaji vyao.

Wengi aliowafunza wangekataliwa na waajiri kama wangeenda kutafuta kazi kwingineko.

Ni hadithi ndefu. Mnamo Agosti 1986, niliona tangazo la kazi ya Mhariri Msanifishaji katika jarida la 'Weekly Review.' Nilikuwa nikifanya kazi kama muundaji na mwelekezi katika Tasisi ya Mafunzo ya Ushonaji Kenya (KTTI) iliyokuwa chini ya Wizara ya Leba.

Wakati huo, sikuwa na mafunzo yoyote kuhusu uanahabari. Niliamua kutuma barua ya kuomba kazi, kutokana na mapenzi niliyokuwa nayo katika uandishi. Nilikuwa pia msomaji sugu wa jarida hilo tangu kuanzishwa kwake mnamo 1975 nilipokuwa Kidato cha Pili.

Nilipendezwa na Hilary nikiwa bado katika shule ya msingi, kutokana na makala yake ya 'Rafiki Yangu Joe' yaliyokuwa na ucheshi mwingi. Makala hayo yalikuwa yakichapishwa kwenye gazeti la 'Daily Nation.'

Wakati Hilary alipogeuza makala yake kuwa jarida la ucheshi liitwalo 'Joe', ilimlazimu baba yangu kuanza kununua jarida hilo kwa ajili yangu. Hilary alikuwa akiandaa jarida hilo akishirikiana na mchoraji vibonzo Terry Hirst.

Alivyoendelea kukaa katika taaluma ya uanahabari, Hilary aligeukia uandishi wa siasa kwa njia pevu, kwenye jarida lililoitwa 'Hilary Ng'weno's Weekly Review.' Niliendelea kumfuatilia kwani sikukosa nakala hata moja ya jarida hilo.

Hebu nirejelee simulizi yangu. Badala ya kuandika barua rasmi ya kuomba kazi, nilibeba nakala ya 'Weekly Review' wakati huo na kuhariri habari kuu. Nilifanya hilo kutoka kwa studio maalumu niliyokuwa nikiitumia kwa kazi zangu za usanifishaji.

Barua yangu ilieleza jinsi jarida hilo lingeweza kuboresha mpangilio wake wa aya. Ni jambo nililoamini lingenisaidia kupata kazi.

Baada ya kumaliza uhariri wangu katika ukurasa huo, niliuweka kwenye bahasha. Nilipokuwa nikienda nyumbani nyakati za jioni, nilipitia katika afisi za jarida hilo katika Jumba la Agip, jijini Nairobi. Niliweka barua yangu chini ya mlango. Sikumwambia Bw Wachira Waruru nilichokuwa nimefanya.



Wakati huo, Bw Waruru, ambaye tulisomea shule moja ya upili, alikuwa Mhariri wa jarida hilo. Kwa mshangao, siku iliyofuata, nilipigiwa simu na Bw Peter Kareithi, aliyekuwa Mhariri wa Habari. Alinialika kufanyiwa mahojiano.

Nilienda siku hiyo hiyo. Nilikutana na Bw Kareithi na Mhariri Mkuu, Bi Sarah Elderkin. Wote walifurahishwa sana na barua yangu. Hata hivyo, walisema kuwa, ikizingatiwa kwamba walikuwa wakitafuta Mhariri Msanifishaji, huenda singefaulu kupata nafasi hiyo. Badala yake walinishauri nijaribu kazi ya uandishi.

Nilikubali ushauri huo. Mtihani wangu wa kazi hiyo ulikuwa kuandika uchanganuzi kuhusu suala la uchaguzi mkuu kwa njia ya 'mlolongo.' Nilitakiwa kurudisha makala hayo siku hiyo hiyo.

Nilijikaza na kurudisha makala hayo Alhamisi hiyo jioni. Ijumaa asubuhi, nilinunua nakala ya jarida hilo na kugundua kuwa Makala yangu ndiyo ilikuwa habari kuu.

Alasiri siku hiyo, nilipigiwa simu. Niliajiriwa kazi kwa mshahara wa wa Sh6,000 kwa mwezi. Hicho kilikuwa kiasi kizuri, ikizingatiwa kwamba kilikuwa karibu mara mbili ya mshahara niliokuwa nikipata katika taasisi ya KTTI. Ilikuwa furaha kubwa kwangu kuanza safari ya uanahabari katika jarida hilo lenye hadhi.

Katika jarida hilo, Hilary alikuwa ameanzisha uandishi wa habari wa kipekee, ambao uliangazia masuala tofauti kwa njia ya kina. Ni mtindo ambao haukuwa umeshuhudiwa katika eneo hili. Kwangu mimi, hiyo ilikuwa nafasi ya kipekee ya kupata mafunzo na tajriba ambayo haingepatikana katika chombo chochote kingine cha habari nchini Kenya.

Ilikuwa furaha kuu kufanya kazi katika chumba cha habari ambako hakukuwa na masharti mengi. Hilary pekee ndiye alionekana kuwa 'bosi' katika chumba hicho.

Hali nyingine ya kipekee ni kuwa hatukuhitajika kuvaa suti au tai, kama inavyohitajika katika afisi nyingi. Watu wengi walidhani kuwa Hilary ndiye alikuwa akiandika jarida hilo peke yake, kwani makala hayakuwa na majina ya waandishi.

Alikuwa akichangia tu nafasi ya 'Barua kutoka kwa Mhariri', kwani aliichukulia kwa uzito sana kama Mhariri Mkuu. Mtindo wake wa kufunza ulikuwa rahisi na wa kipekee. Alikuwa akiwafunza wanahabari mtindo wa kuboresha uandishi wao kupitia kazi zao na kuwapa mapendekezo kuhusu jinsi ya kuboresha kazi zao.

Jarida hilo lilifungwa mnamo 1999, baada ya kupata umaarufu mkubwa katika jukwaa la uanahabari. Licha ya kufungwa kwake, lilitoa mchango mkubwa sana katika ukuaji wa uanahabari nchini.

Hilary alianzisha taaluma yake katika Shirika la Nation. Alirudi Kenya baada ya kusomea Fizikia katika Chuo Kikuu cha Havard. Alirudi nchini punde tu baada ya Kenya kupata uhuru wake. Aliweka historia kwa kuteuliwa Mhariri Mkuu wa gazeti la 'Daily Nation' akiwa na umri wa miaka 25 pekee. Alikuwa Mwafrika wa kwanza kuhudumu katika nafasi hiyo. Hata hivyo, aliondoka baada ya chini ya mwaka mmoja.

Hajawahi kueleza sababu halisi ya kujiondoa kwenye wadhifa huo, ijapokuwa kumekuwa na uvumi kuwa hakufurahia kuhudumu katika nafasi hiyo wakati wa utawala ambapo walowezi kutoka Uingereza walikuwa wakimfuata kila mara.

Kwenye uandishi wake, Hilary alizamia masuala tofauti kwa kina, bila kuweka hisia zake. Ni vizuri kutaja kuwa kifo chake mwaka uliopita kiliashiria mwisho wa mojawapo ya wahariri wa kizazi kilichoanzisha na kukuza taaluma ya uanahabari nchini.

Wahariri wakuu wengine ambao walijizolea umaarufu sawa na huo ni George Githii (aliyehudumu mara mbili katika Nation Media Group na mara moja katika Standard Group), Henry Gathigira (Standard) na Philip Ochieng', aliyefariki mwaka uliopita, karibu wakati sawa na Hilary.

Hiyo haina maana hakujawa na wahariri wakuu wengine stadi nchini. Kufikia sasa, kuna wahariri wanaoendesha na kusimamia mtindo mpya wa uanahabari nchini. Ni wahariri wenye ujuzi mkubwa wa kielimu na kitajriba kuliko watangulizi wao.

Hata hivyo, wengi bado hawatambuliwi na wasomaji, ispokuwa wafanyakazi wenzao.

Wenyeviti wa bodi, maafisa wakuu watendaji, wakurugenzi wakuu na wasimamizi wa mauzo ndio wanaotambuliwa kama sura na sauti za vyombo vya habari.

Idara za uhariri hazina usemi na muonekano mkubwa kama ilivyokuwa awali. Nyingi zimefichwa kutokana na sababu za kibiashara na kisiasa.

Mwelekeo huo umeathiri sana uhuru wa uhariri, kwa kiwango ambacho Hilary na watangulizi wake hawangefurahia.

kurunzi ya Kenya

■ MAADILI YA KIDINI YA TAIFA

# KANISA MSALABANI

*Nyakati zimebadilika na mbinu za hali ya kisiasa na mawasiliano imebadilika. Lakini wajibu wa kanisa la Kristo haujabadilika. Je, kanisa linatekeleza jukumu lake la kuhakikisha uongozi mwema?*

● Na KWENDO OPANGA


Usiku wa pili wa kuhesabu kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi uliopita, Wakenya wengi walishangaa kuona viongozi kadhaa wa makanisa na kwaya za kiroho katika ukumbi wa Bomas of Kenya, kituo cha kitaifa cha kujumulisha matokeo ya kura za urais.

Watangazaji wa runinga katika studio na wenzao waliokuwa wakiripoti kutoka Bomas walielezea mshangao wao. Waliulizana, wakishangaa, kile ambacho Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), ambayo ni msimamizi wa uchaguzi, ilikuwa imepanga. Kwa nini Mwenyekiti wa Wafula Chebukati na wenzake wapange kupatia hadhira yao mahubiri na muziki, badala ya kuwafahamisha hali ya ujumuishaji wa matokeo ya urais kutoka vituo vya kura vya kaunti zao kote nchini?

Picha za matukio mengine zilitumwa upesi katika studio. Ilikuwa wazi kwamba Wakenya na wanahabari wa runinga waliokuwa wakishangaa hawakuzingatia ripoti nyingi kutoka seheme mbalimbali nchini za viongozi wa kidini waliokutana chini ya mwavuli wa mashirika tofauti kuombea amani idumu wakati wa kampeni na kwenye uchaguzi mkuu wa Agosti 2022.

Siku nne baadaye, mnamo Agosti 15, wanahabari na watazamaji walikuwa wamezoea kwaya na viongozi wa kidini. Wote, wakiwemo viongozi wa vyama waliodhinishwa na wafuasi walikuwa na kiu ya habari. Lakini wasiwasi ulionekana wazi miongoni mwa wanahabari kuliko wanakwaya na viongozi wa kidini waliokuwa wametulia. Umuhimu wao ulionekana wazi na ushahidi ulikuwa hapo kwa kila mtu kuutazama. Wakiwa chini ya mashirika mapya na ya zamani, viongozi wa kidini Kenya walikuwa wamejiandaa na wenzao kwa siku au usiku wa uchaguzi waliotakiwa kuwa watulivu, wenye amani na kuungana kuwa kitu kimoja. Na viongozi hao wa kidini hawakuhutubia waumini wao pekee au Wakenya wa kawaida, walilenga pia viongozi wakuu wa kisiasa Kenya. Hebu msikilize Pasta Patrick Kuchio wa Christ Is the Answer Ministries (CITAM), Valley Road, Nairobi.

"Viongozi wa kidini hawakutaka kupatikana ghafla bin vuu kama ilivyokuwa wakati wa ghasia za uchaguzi wa 2007. Walitaka kuhusika na siasa za uchaguzi kama wapatanishi, washiriki, raia, walinzi na watetezi wa amani. Wanafaa kuhubiria waumini wao na pia kuzungumza na kushauri viongozi wakuu wa kisiasa Kenya."



Askofu Mkuu Ndingi Mwana a'Nzeki mnamo Julai 31, 2009.

Kwa mfano, anasema Kuchio, kukutana na kumshauri Rais Kenyatta na kumpatanisha na wagombeaji urais, kulitengewa viongozi mashuhuri wa makanisa kama David Oginde wa CITAM, Mkuu wa Kanisa Kiangilikana nchini, Askofu Mkuu Jackson ole Sapit na Askofu Mkuu Antony Muheria wa Dayosisi ya Nyeri ya Kanisa Katoliki miongoni mwa wengine.

**Kampeni za amani**

Sio sadfa kwamba tangu Agosti 15, Chebukati alipotangaza Naibu Rais William Ruto kuwa Rais Mteule na matukio yaliyofuata tangu wakati huo, Muheria, Sapit, Oginde na Hassan ole Naado wa Baraza Kuu la Waislamu Kenya, wakiandamana na wengine wengi, wamekutana na Rais Kenyatta, Ruto na Bw Raila Odinga. Na viongozi wa kidini walikuwa wakizungumza, kushauri na kuweka makubaliano ya amani na viongozi wa maeneo tofauti humu nchini.

Dkt Isaac Wekesa Wawire, Askofu, mhadhiri na mwandishi wa vitabu anayehudumu katika Kaunti ya Vihiga anasema: "Viongozi wa kidini katika kaunti walikutana na wagombeaji wote wa uchaguzi akiwemo Gavana Wilbur Ottichilo na wapinzani wake na kuzungumza kuhusu amani na maendeleo katika kaunti yetu. Tulikula kiamsha kinywa na wagombeaji wa ugavana na wakatia saini mkataba wa kudumisha amani na kufanya kampeni za amani, midahalo katika runinga na kuheshimu matokeo ya uchaguzi."

Kulikuwa na juhudi za kimataifa pia. Kuanzia Juni 16 hadi 18 mwaka wa 2021, viongozi zaidi ya 400 wa kidini walikutana katika hoteli ya Movenpick, Westlands, Nairobi, wengine 3,000 walihudhuria kwa njia ya video na wote walitoka katika mataifa 53 kujadili jukumu la viongozi wa kidini katika uchaguzi uliokamilika majuzi Kenya.

Kuanzia hapo, msingi uliwekwa wa jukumu ambalo viongozi wa kidini Kenya walitekeleza

# kurunzi ya Kenya

vyema kwa kuweka amani katika ajenda, katika kura au katika moyo wa uchaguzi mwezi jana na katika kampeni zilizoutangulia. Msikilize Kuchio tena. "Tumetumia saa nyingi sana na viongozi wa kidini, kuzungumza, kujadiliana, kuwashawishi na kuhakikishiana tena na tena."

Je, ni kweli, kama wanavyoamini watu wengi, kwamba kwamba viongozi wa sasa wa kidini Kenya wameacha msimamo mkali wa watangulizi wao wa miaka ya sabini, themanini na tisini ambao walikuwa wakiwakabili ana kwa ana wanasiasa katika kutetea wanyonge?

Majina kama Padri Timothy Njoya, mwenzake wa Baptist Mutava Musyimi na marehemu maaskofu David Gitari, Henry Okullu na Alexander Muge pamoja na Askofu Mkuu Ndingi Mwana a'Nzeki, yanakuja akilini. Akizungumza kwa niaba yake binafsi, Padri Ernest Eshamwata, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa kanisa la Church of God in East Africa, misheni ya Kima, anasema kuwa ana maoni tofauti. "Nyakati zimebadilika na mbinu za mawasiliano zimebadilika. Lakini jukumu la unabii na maono ya kanisa hayajabadilika. Baraza la Kitaifa la Makanisa Kenya (NCCK), huzungumza, husimama na kututetea na kama kanisa, pia tunatekeleza majukumu yetu ya unabii."

Kwa njia nyingine, viongozi wa makanisa wakati huu, sawa na watangulizi wao waliokuwa na bidii ambao wametajwa hapo juu, wanajua na kutambua kwamba kanisa ndilo dhamiri ya maadili ya taifa. Lakini tofauti na watangulizi wao waliopigana vikali na wanasiasa, mikakati, vifaa na majukwaa ya mazungumzo yamebadilika. Kuchio anaongeza kuhusu mtazamo huu.

### Kupigana na umasikini

"Wao (Njoya na wenzake) walihudumu chini ya utawala wa chama kimoja wakati demokrasia ilikuwa imekadamizwa. Demokrasia imepanuliwa kwa kiwango kikubwa. Hali ya mawasiliano haikuwa imestawi na kuwa ilivyo wakati huu. Hawakuwa na njia nyingi za mawasiliano. Walikuwa wakitetea wanyonge kutoka makanisa yao binafsi. Siku hizi makanisa yanazungumza pamoja."

Wawili hao wanasema ukweli. Nani angesema ndiye msemaji hapa?

"Juhudi zako za kupigana na ufisadi Kenya zimeshindwa. Ni viongozi wachache sana jasiri Kenya ambao hawataki kulaumiwa kwa chochote?" Na hapa?

"Ufisadi uko katika midomo ya kila mtu, lakini pia uko katika mikono ya Wakenya wengi. Hata janga limekuwa nafasi ya kupora masikini na kuibia nchi." Hizi ni nukuu kutoka kwa ripoti ya NCCK inayoitwa Maoni kutoka kwa Viongozi wa Kidini wakati wa Mkutano na Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta kuhusu Hali ya Nchi. Iliandikwa Septemba 25, 2020 na kukabidhiwa Rais katika Ikulu ya Nairobi siku nne baadaye.

Viongozi wa Kidini walikuwa Ikulu kwa mwaliko wa Rais. Huenda maneno yao hapo juu yalitamkwa na Njoya na wenzake katika siku walizokuwa wakikabili serikali lakini ni vigumu kufikiri saba waliotajwa hapo juu wangealikwa kwa hotuba au kuruhusiwa kumshauri Rais Moi.

La muhimu ni kwamba, ripoti ya NCCK inasema kwamba "mkutano huo uliwakilishwa na imani tofauti za kitamaduni na mashirika tofauti ya kidini" na uliwakilisha "dhamiri ya maadili ya nchi", kwa sababu "nchi inayoacha roho wa Mungu au kukataa kuzungumza na sauti za kiroho kila wakati, ni nchi isiyo na moyo."

Kwa ufupi, Wawire anasema, katika kutekeleza wajibu wao katika Uchaguzi Mkuu wa 2022, viongozi wa Kidini:

"Hatukuegemea upande wowote kama makanisa binafsi au wanachama wa mshirika ya makanisa. Usitenganishe viongozi wa kidini na wanasiasa kwa kuwa sisi sote ni Wakenya na wanasiasa pia ni waabudu. Dhana kwamba hatutetei wanyonge si ya kweli."

kutoka UK 9

wapiganiaji uhuru ulipokuwa ukiendelea. Alipoachiliwa huru, alitumwa kukutana na mume wake Mararal, ambako Jomo alikuwa akihudumia kifungo cha nyumbani.

Aliondoka na binti yake, aliyejiunga na Shule ya Msingi ya Mararal DEB, huku mdahalo ukiendelea Uingereza kuhusu hatima ya Kenyatta kisiasa. Serikali ya wakoloni ilikuwa kwa kawaida ikimtuma Dkt Arnold Carvalnho kuchunguza familia hiyo. Ripoti iliyotumwa Julai 1961 kuhusu familia ya Kenyatta ilisema kwamba Mama Ngina alikuwa na "mimba ya wiki 26. Alitarajiwa kujifungua Novemba 4, 1961...na angeweza kusafiri salama angani."

Mnamo Agosti 14, 1961, Mama Ngina alisafirishwa kwa ndege akiandamana na "polisi mlezi" na mnamo Oktoba 26, akajifungua Uhuru Kenyatta.

Wakati wa sherehe za kuadhimisha Uhuru wa Kenya, vyombo vya habari vya Magharibi vilipigwa na butwaa "Bi Kenyatta wa 3" alipokwenda katika Uwanja wa Ndege wa Embakasi kumkaribisha "Bi Kenyatta wa 2", wakimaanisha mke wa pili wa Jomo, Edna, ambaye ni raia wa Uingereza, "kisha wote wawili wakaandamana kwa furaha kumlaki mume wao – Waziri Mkuu wa Kenya.

Akiwa mke mchanga zaidi katika familia yenye wake wengi, Mama Ngina alikuwa nguzo muhimu Kenyatta alipokuwa akijiandaa kuchukua mamlaka ya utawala.

Si mengi yanayofahamika kuhusu ukaribu wake na Rais na ni kwa kiasi kipi alichoathiri maamuzi katika Ikulu ya Jomo, ingawa historia ya Afrika inasheheni matukio ya siri na majukumu yasiyo ya kawaida ya kisiasa yanayotekelezwa na Wake za Marais.

Lakini ni katika ununuzi wa ardhi baada ya uhuru uliosababisha Mama Ngina kulengwa na wakosoaji. Notisi rasmi zilizochapishwa Kenya katika miaka ya 1960 na 70 kuonyesha baadhi ya mali zilizonunuliwa na familia hiyo kwa jina la Mama Ngina au wanawe wawili wakubwa wa Kenyatta - Peter Magana na Peter Muigai.

Kwa mfano, hata kabla ya kumaliza mwaka mamlakani, mnamo 1965, Mama Ngina alinunua ekari 1,006 za ardhi eneo la Dandora kutoka kwa Bwana Hendrik Rensburg kwa gharama ya Sh200,000 – ambazo zilikuwa pesa nyingi sana enzi hizo. Kenyatta alipokuwa na shughuli nyingi au alipougua, ni Mama Ngina aliyekuwa akimtunza. Isitoshe, alikuwa nyumbani kwake Gatundu kila mara pamoja na watoto.

Mnamo 1977, vyombo vya habari vya Magharibi vilimshutumu Mama Ngina kwa kujihusisha na biashara haramu ya pembe za ndovu iliyokuwa tayari imepigwa marufuku Kenya. Lakini jinsi baadaye ilibainika kuwa ni kampuni ya binti yake wa kambo, Margaret Wambui, United Africa Corporation, shirika linalonunua bidhaa mbalimbali kutoka mataifa ya kigeni, iliyohusika na biashara hiyo.

Lakini ikizingatiwa kuwa Mama Ngina



Rais Kenyatta na Mama Ngina wakichesherehekea Mwaka katika Mpya Ikulu ya Mombasa.


hakuwahi kujitetea, shutuma kama hizo zilimwacha hoi mikononi mwa mahasimu wake. Kenyatta aliaga dunia Mama Ngina akimwangalia usiku wa Agosti 22, 1978. Wakati huo alikuwa na umri wa miaka 45. Mamlaka yalipoanza kumponyoka, alirudi nyumbani kwake Gatundu, akajenga nyumba Muthaiga, na kudumisha makao karibu na Ikulu. Huku Ikulu ikiwa na wapangaji wapya, Mama Ngina aliimarisha himaya ya Kenyatta kwa kuwekeza katika ustawishaji, kilimo na sekta ya hoteli. Aidha, aliuza mapande ya ardhi iliyokuwa imenunuliwa na Kenyatta – ingawa bado alibaki na ekari nyingi – zilizotosha kuifanya familia hiyo kumulikwa vibaya.

Kabla ya Uhuru Kenyatta kujitosa kwenye ulingo wa siasa na kupitia ushawishi kutoka kwa mama yake, familia ya Mama Ngina ilikuwa imejitenga na siasa za mfumo wa vyama vingi zilizokuwa zikichipuka nchini.

Alijitenga kabisa huku wandani wake wakikumbana na ghadhabu ya utawala wa Kanu. Kando na enzi za Kanu ya Kenyatta, ni vigumu kujua msimamo wake wa kisiasa – ilhali angali amesalia kigogo mashuhuri wa kisiasa mwenye rasilimali za kutosha kuwafadhili wagombea wa kisiasa. Ni baada tu ya mwanawe kuhusishwa na ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007 ambapo Mama Ngina aliitisha maombi hadharani. Picha yake akimuombea mwanawe ilihidhirisha wazi uhusiano kati yake na siasa za humu nchini.

Ajabu ni kuwa, hata baada ya Uhuru kushinda urais, ameendelea na maisha yake ya kawaida. Watu waliodhani Mama Ngina wa miaka ya 70 angejitokeza na Uhuru walishangaa. Kiwango cha mamlaka anayosheheni ni cha kukisiwa tu. Iwapo kweli yeye ni mkono usioonekana ni suala linaloweza kuamuliwa kutokana na jinsi anavyotangama na siasa za humu nchini. Je, amejitenga? La, bila shaka.

## Sayansi na Teknolojia




# NASA: 'SIJAWAHI KUONA JUPITA NAMNA HII'

*Darubini hunasa picha za kipekee za miale ya kaskazini na kusini mwa Jupita. Sehemu yake kubwa nyekundu, kilinge kikubwa kiasi cha kuweza kumeza dunia, inachomoza kwa mwangaza mkali ikiandamana na vilinge vingine vingi. Picha moja pana inajitokeza kwa namna ya kipekee ikionyesha viduara hafifu karibu na sayari hiyo.*

• AFP

Darubini ya Nasa James Webb imenasa picha za kustaajabisha za sayari ya Jupita zinazoonyesha miezi miwili midogo, pete na miale hafifu katika ncha za Kaskazini na Kusini.

"Hatukutarajia iwe bora kiasi hiki, kwa hakika," anasema mnajimu wa kuchunguza sayari, Imke de Pater, kutoka Chuo Kikuu cha California, Berkeley. "Inapendeza mno kwamba tunaweza kuona kwa kina vitu kwenye Jupita ikiwemo pete, vijisatelaiti na hata galaksi katika picha moja," akasema.

De Pater aliongoza uangalizi wa Jupita, ambayo ndiyo sayari kubwa zaidi katika mfumo wetu wa jua, pamoja na Thierry Fouchet, wa Kituo cha Unajimu cha Paris.

Picha hizo zilinaswa kupitia kamera aina ya Near-Infrared za kituo hicho (NIRCam) na zilipakwa rangi kwa sababu mwangaza wake hauwezi kuonekana kwa jicho la binadamu.

Miale iliyopo juu ya pembe za kaskazini na kusini mwa Jupita imechorwa kwa rangi nyekundu zaidi huku Sehemu Kuu Nyekundu, dhoruba iliyo kubwa kushinda Ardhi, ikionekana kuwa nyeupe.

Picha moja inaonyesha pete hafifu za Jupita na miezi yake Amalthea na Adrastea.

Tangu ilipozinduliwa Disemba mwaka jana kutoka French Guiana kwenye roketi ya Ariane 5, Webb inazunguka Jua kutoka umbali wa maili milioni (kilomita 1.6 milioni) kutoka kwenye Dunia, katika eneo tupu linaloitwa Lagrange Point.

Ilichukua chombo hicho karibu mwezi mmoja kufika eneo hilo, ambapo kimesalia katika nafasi moja nyuma ya Dunia na Jua ili kupata taswira nzuri ya maumbile ya sayari.

Darubini ya Webb ni ushirikiano wa kimataifa kati ya shirika la kuchunguza sayari la Amerika, Nasa, Shirika la Sayari la Uropa, Shirika la Sayari la Canada, unaojumuisha zaidi ya watu 10,000.

# Kwa nini mbwa hutokwa na machozi wanapoungana tena na wenyeji wake

Wanaomiliki mbwa wanajua vyema furaha isiyo kifani ya kurudi nyumbani baada ya safari ndefu na kulakiwa na mfugo wao huku akichezesha mkia, kuruka bila kujizuia na kuramba nyuso zao.

Lakini wanyama hao waliojawa na furaha huenda wanamwaga mengi zaidi ya manyoya kwenye nguo zako – huenda wanabubujikwa na machozi, kulingana na utafiti mpya uliochapishwa wiki iliyopita katika jarida la 'Current Biology'.

"Hatujawahi kamwe kusikia uvumbuzi kuwa wanyama hutiririkwa na machozi ya furaha katika matukio kama hayo, kama vile kuungana tena na wenyeji wao," akasema Takefumi Kikusui, mmoja kati ya waandishi wa utafiti huo alioutaja kuwa unaoweza kuwa wa "kwanza duniani."

Mwanasayansi huyo alipima kiasi cha machozi kwenye macho ya mbwa kupitia kipimo kinachotumika mno cha Schirmer, ambacho huhusisha kuweka kifaa maalumu chini ya kope.

Kwa matokeo ya kuwezesha ulinganishi, walichukua vipimo hivyo kutoka kwa mbwa wakati wa kutangamana kwa kawaida na wenyeji wao. Mbwa walipoungana na wenyeji wao baada ya saa tano hadi saba za kutengana, waliongeza "pakubwa" kiwango cha machozi katika muda wa dakika tano zilizofuata, watafiti walibaini.

Aidha, waligundua kuwa kiasi cha machozi kutoka kwa mbwa hao kilikuwa cha juu zaidi walipoungana tena na wenyeji wao ikilinganishwa na watu wengine ambao mbwa husika amezoeana nao.



# kurunzi ya Afrika

■ UMEME KUPOTEA NI KAWAIDA KATIKA TAIFA HILO



Wenye biashara kando ya wakiuza bidhaa zao sokoni bila stima mjini Ibafo, Jimbo la Ogun, kusini-magharibi ya Nigeria, Machi 22. Kupotea kwa umeme ni jambo la kawaida katika nchi hiyo inayoongoza barani Afrika kwa kutoa mafuta, ambapo miundomsingi iliyoporomoka mara nyingi hushindwa kusambaza hata umeme usio wa kutosha. Kuporomoka kwa usambazaji umeme na bei za juu za mafuta ulimwenguni zimesababisha upungufu mbaya zaidi wa nishati nchini humo. Biashara nyingi hutegemea mafuta ya dizeli kwa taa umeme ukipotea. PICHA I AFP

# NIGERIA, NCHI YA GIZA

*Taa zimezimika katika taifa lenye idadi kubwa la watu barani Afrika. Visa vya kupotea kwa umeme hutokea kila mara kutokana na kuyumba kwa uwezo wake wa uzambazaji stima. Taifa hilo linaloongoza katika uzalishaji mafuta barani Afrika pia linakumbwa na shida ya ukosefu wa uwezo wa kuzalishaji umeme wa kutosha na usambazaji wa kawi hiyo.*

MOSHI mweusi mkali unatualika katika soko la fanicha katika kituo cha kibiashara cha Kugbo kilichoko viungani mwa jiji kuu nchini Nigeria, Abuja.

Moshi huo kutoka kwa majenereta unawasha mapua ya watu katika kituo hicho cha kibiashara karibu na mji wa Nyanya - umbali wa kilomita sita kutoka jiji la Abuja.

Muda mfupi baadaye, sauti kali inatoka kwa mashine na kugonga masikio yetu huku nusu ya zaidi ya watengenezaji fanicha 128 wakianza kazi.

Shughuli katika viwanda vilivyo katika kituo hicho cha kibiashara zilikuwa zimesimama kwa karibu siku tatu baada ya umeme kupotea katika eneo pana la Karu, lenye miji midogo mingi inayopakana na Abuja.

Baadhi ya wateja wanaonekana wakifunika nyuso zao kwa kutumia barakoa au vitambaa kuepuka kuvuta moshi wenye sumu kali.

Machozi yanatoka machoni mwao kwa sababu ya gesi zenye kemikali hatari, zilizoenea angani. Hata hivyo, baadhi yao wanaonekana kuvumilia hali hiyo ngumu huku wakisikika wakiwasiliana na wauzaji fanicha hizo kwa sauti ya juu.

Wauzaji hao wanaonekana kana kwamba wamezoea hali ngumu katika soko hilo.

Changamoto zinazoshuhudiwa katika kituo cha kibiashara cha Kugbo ni kielelezo cha shida ambayo imekumba Nigeria tangu ipate uhuru; kupotea kwa umeme kila mara na maeneo mengine kukosa kufikiwa na umeme.

Licha ya kuwa nchi yenye utajiri wa kima cha dola 515 bilioni za Amerika (Sh68.8 trilioni) na hivyo kuorodheshwa kama taifa tajiri zaidi Afrika Magharibi, Nigeria imegeuka kuwa "taifa la jenereta".

**Umeme hupatikana kwa muda usiozidi saa nne kwa siku, huku kampuni ya kusambaza umeme nchini humo ikiwasha stima sehemu fulani na kuzima katika sehemu zingine kwa zamu.**

Nyumba za makazi, maduka, shule, hospitali na viwanda vinaendesha shughuli zake kwa umeme kutokana na jenereta.

Vijiji, masoko, miji midogo na mikubwa, likiwemo jiji la kibiashara la Lagos, hushuhudia ukosefu wa umeme, kutoka kwa hifadhi ya kitaifa kwa siku nyingi au hata wiki kadhaa.

Na hatimaye umeme ukirudi hudumu kwa muda usiozidi saa nne kwa siku. Hii ni kwa sababu Kampuni ya Usambazaji Umeme Nigeria (TCN) inatekeleza mpango wa utoaji stima kwa vipimo; kwa kuwasha maeneo fulani na kuzima katika mengine kwa zamu.

Hali hii ya kupotea kwa stima kila mara na ugavi wake kwa vipimo umeathiri uchumi wa Nigeria kwa kiwango kikubwa sana.

Wawekezaji na wataalamu wanasema hali hi-

...Endelea Uk 26

kurunzi ya Afrika

# Huwezi kuishi bila jenereta nchini Nigeria



Vijana wakitengeneza jenereta katika karakana eneo la Bulabulin, jimbo la Maiduguri, Februari 1, 2021. Wakazi wa kaskazini - mashariki ya mji wa Maiduguri, Nigeria walikabiliwa na kupotea kwa umeme kwa wiki kadhaa baada ya wanamgambo kulipua vifaa vya usambazaji na pia kusababisha shida ya maji, kuvuruga biashara na maisha ya wakazi. Uvamizi huo ulikuwa wa tatu ambao kundi hilo linalohusisha na IS lilitumbukiza mji mzima gizani kwa siku kadhaa kwa kulipua vifaa vya kusambaza umeme. PICHA I AFP

...Kutoka Uk 25

yo imefanya uchumi wa nchi kuyumba na wafaUmenyabiashara kupata hasara.

Katika soko la Kugubo, kwa mfano, maseremala hukaa bila kazi kwa wiki kadha kutokana na ukosefu wa nguvu za umeme na mbao.

Hali hiyo pia huchangiwa na gharama ya juu ya dizeli ya kuendesha jenereta zao kuukuu.

"Sasa ni vigumu kwetu kukamilisha seti moja ya fanicha katika muda wa wiki mbili. Zamani tungekamilisha kazi hiyo kwa siku mbili. Tumeshindwa kununua dizeli kwa sababu bei yake iko juu, gharama ambayo hatutaki kupitisha kwa wateja wetu," anasema Chucks Ude, mmiliki wa duka la fanicha kwa jina Big Time Furniture.

Bei ya dizeli imepanda kwa kiwango kikubwa kwani lita moja inauzwa kwa Dola 1.93 za Amerika (Sh231.6) kutoka dola 0.8 (Sh96) mwaka mmoja uliopita.

Bei ya petroli pia iko juu kiasi kwamba wengi wa wamiliki wa viwanda hawawezi kuimudu.

Okolo Anslem, Afisa Mkuu wa kiwanda cha OK Furniture, anasema uhaba wa mbao umeendelea kushuhudiwa kwa sababu wapasuaji mbao wanakosa umeme wa kuendesha mitambo ya kupasua magongo.

Katika Kampuni ya Akin Ola Sawmilling, saa za kazi zimepunguzwa kwa siku huku mwenye kampuni akitaka kupunguza hasara kwa kutumia dizeli ghali kuendesha jenereta kubwa.

"Unaona idadi kubwa ya magongo katika karakana yetu. Hatuwezi kuyapasua kupata mbao za saizi tofauti au kuyachonga ili wateja wanunue," akasema Akin Olaosebikan, Afisa Mkuu Mtendaji wa kampuni hiyo. "Tumekuwa tukihudumia watengenezaji fanicha na wajenzi lakini sasa hatuwezi kukidhi mahitaji yao," anaongeza.

Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Wafanyabiashara na Wamiliki wa Viwanda, mjini Lagos, Muda Yusuf, anasema shida ya nguvu za umeme imechangia kupanda kwa gharama ya kufanya biashara na kuwavunja moyo wawekezaji wa kigeni.

"Gharama ya juu ya kutoa umeme mbadala yamkini ni mojawapo ya shida zinazodumaza ukuaji wa viwanda nchini Nigeria. Hii imefanya viwanda vyetu kupata hasara kubwa katika siku za hivi karibuni," anaongeza.

Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) limetaja ugumu wa kupata stima na usambazaji usiotegemewa wa kawi kama sababu kuu inayoathiri uendeshaji wa biashara nchini Nigeria.

Hali hiyo imechangia hasara ya kima cha dola 29 bilioni (Sh340 bilion) kwa nchi.

Ripoti ya IMF inasema licha ya kwamba Nigeria huzalisha mafuta na gesi kwa wingi, ni mojawapo ya nchini zinazokubwa na uhaba mkubwa wa kawi duniani.

"Kampuni za kusambaza umeme hupoteza pesa nyingi kwa sababu sehemu ya kawi hiyo hupotea kutokana na miundo mbinu mbovu ya kuisambaza na wizi. Hasara nyingine inatokana na hali kwamba wateja wengine hawalipi bili zao," inasema sehemu ya ripoti hiyo ya IMF.

"Sita kati ya wateja 10 ndio waliosajiliwa kwa hivyo bili zao za stima hazifahamiki kwa urahisi. Hali hii inachangia wateja wengi kukosa kulipa bili za stima." inaongeza.

Hali imeendelea kuwa mbaya katika nchi ambayo imeshikilia nafasi ya sita miongoni mwa zinazotoa mafuta kwa wingi. Usambazaji wa umeme, ambao huendeshwa na shirika la TCN, ambalo hukusanya na kusambaza umeme wote unaozalishwa na kampuni mbalimbali (GenCos), umekwama mara sita mwaka huu.

Kwa mfano, mnamo Julai 20, hali hiyo ilitokea na kuchangia umeme kupotea kote nchini.

Mageuzi mbalimbali yanayotekelezwa katika sekta ya kawi hayajaimarisha hali licha ya kuundwa kwa kampuni 23 za kuzalisha umeme.

Kampuni hizo zinasimamiwa na watu binafsi na Kampuni ya Niger Delta Holding.

Mkataba wa Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na ile ya Kibinafsi ulichangia kugeuzwa kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Umeme (Nepa) kuwa kampuni ya Power Holding Company of Nigeria (PHCN) ili iweze kubinafsishwa.

Sheria kuhusu Mageuzi katika Sekta ya Kawi ilitungwa mnamo 2005 na ikagawanya kampuni ya PHCN katika vitengo 18: kampuni 11 za usambazaj; kampuni 23 za uzalishaji umeme na moja ya kupitisha umeme wa kiwango cha juu.

Mageuzi haya yameshindwa kuwezesha makazi nchini Nigeria kuwa na umeme na yamechangia ongezeko la visa vya kupotea kwa umeme kila mara.

Hali hiyo imepiga jeki biashara ya uagizaji wa jenereta kutoka mataifa ya nje. Huku hitaji la umeme nchini Nigeria likiwa megawati 40,000, wakati huu kampuni hizi zinazalisha chini ya megawati 5,000.


Hali hii imewaacha mamilioni ya raia wa Nigeria kusaka mbinu mbadala za kupata umeme na sasa karibu kila mtu amegeukia jenereta.

Kulingana na mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) tawi la Nigeria Ebrima Faal, raia wa nchi hiyo walitumia karibu dola 14 bilioni (Sh168 bilioni) mnamo 2021 kununua jenereta na mafuta ya kuziendesha.

Kiwango hiki cha fedha kinawakilisha ongezeko la dola 2 bilioni (Sh24 bilioi) zaidi ya kiwango walichotumia mnamo 2020.

# kurunzi ya Dunia

■ CHAMA CHA CONSERVATIVE CHAPATA KIONGOZI MPYA



Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Uingereza Liz Truss akijibu maswali wakati wa hafla ya Chama cha Conservative mjini Birmingham, Agosti 23.
PICHA | AFP

# Truss ndiye Waziri Mkuu mpya

*Wanachama wa Conservative waliomchagua Waziri Mkuu mpya wa Uingereza weupe wakongwe. Karibu thuluthi mbili ni wanaume.*

● AFP

Chama cha Conservative nchini Uingereza Jumatatu kilimtangaza Liz Truss kuwa kiongozi mpya kumrithi Waziri Mkuu Boris Johnson na kukabiliana na hali mbaya ya kiuchumi ambayo haijawahi kushuhudiwa nchini humo kwa miaka mingi.

Truss, ambaye ni Waziri wa Mashauri ya Kigeni, alimshinda kwa urahisi mpinzani wake, aliyekuwa Waziri wa Fedha, Rishi Sunak, kwa asilimia 57 ya kura kufuatia ushindani mkali ambao uliamuliwa na wanachama 170,000 wa Chama cha Conservative – sehemu ndogo sana ya wapiga kura wa Uingereza.

Katika hotuba yake fupi ya ushindi mjini London, Truss alisema ni 'heshima' kwake kuchaguliwa baada ya kufanya 'mmoja wa mitihani mrefu zaidi ya kikazi katika historia".

Truss, 47, atakuwa mwanamke wa tatu nchini Uingereza kuhudumu kama Waziri Mkuu baada ya Theresa May na Margaret Thatcher.

Alianza kazi rasmi Jumanne baada ya Johnson kuwasilisha barua yake ya kujiuzulu kwa Malkia Elizabeth II.

...Endelea UK 28

kurunzi ya Dunia

# Truss hatimaye achaguliwa Waziri Mkuu mpya wa Uingereza

...Kutoka Uk 27

Truss amerithi uchumi ambao unatarajiwa kuingia awamu mbaya zaidi mwishoni mwa mwaka.

Wakati wa kampeni zake, Truss aliahidi kupunguza kodi huku Uingereza ikishuhudia mfumko wa bei za bidhaa ambao mara ya mwisho ulioneka miaka 40 iliyopita.

Aliahidi pia kubatilisha ongezeko la hivi majuzi la malipo ya bima ya kitaifa kwa wafanyakazi ambayo hugharamia afya ya umma na msaada wa wasiojiweza.

Truss pia anapendekeza kupunguza kodi za mafuta inayotumiwa kudhamini mpango wa nishati isiyochafua mazingira.

Bajeti ya dharura inatarajiwa wiki chache zijazo , huku Banki Kuu ya Uingereza (BoE) ikitabiri kwamba Uingereza itaingia kipindi cha mwaka mzima cha kushuka kwa uchumi mwishoni mwa 2022.

Kabla ya hapo, Truss anatarajiwa kutoa mpango wa kukabiliana na bei zinazoendelea kupanda za nishati.

"Nikichaguliwa waziri mkuu, nitashughulikia mara moja bei na usambazaji wa nishati," Truss akaambia shirika la habari la BBC mnamo Jumapili.

Wakati wa kampeni, Truss alitaja kupanda kwake hadi ngazi ya juu kisiasa Uingereza kuwa "safari" ambayo imemfanya kulaumiwa kwa kuwa na tamaa ya kutumia kila nafasi inayomjia. Anatoka familia ya mrengo wenye msimamo mkali kisiasa na mwanzoni alijiunga na chama cha msimamo kadiri cha Liberal Democrats kabla ya kuhamia chama cha Conservative. Alichaguliwa mbunge wa eneobunge la South West Norfolk, mashariki ya England mwaka wa 2010, na kunusurika ufichuzi wa uhusiano ambao karibu umgharimu uteuzi wake.

Tangu 2012 ameshikilia msururu wa nyadhifa za uwaziri katika wizara za elimu, fedha na idara na vile vile alikuwa na kipindi kigumu katika wizara ya haki. Mwaka wa 2016, alishiriki kampeni ya Uingereza kubaki katika Muungano wa Ulaya lakini kwa haraka akawa mmoja wa waliotetea Brexit wakati Waingereza wengi walipinga kura kuondoa nchi yao katika muungano huo. Uingereza ilipojiondoa EU, Johnson alimteua kusimamia mazungumzo kuhusu mikataba mipya ya kibiashara kabla ya kumteua Waziri wa Mashauri ya Kigeni mwaka jana.

Katika wadhifa huo, alichukua jukumu lililozua utata la kujaribu kuondoa kabisa tofauti na Brussels kuhusiana na biashara baada ya Brexit katika Ireland Kaskazini. Sawa na Johnson,Truss amekuwa mkali kuhusu Urusi na kuunga Ukraine bila kuyumba.



**2016**

Kura ya maamuzi Uingereza mnamo 2016 iligawanya wapiga kura asilimia 52 kwa 48 kuunga mkono hatua ya Uingereza kutoka Jumuia ya Ulaya.

## 'Kamaliza Boris Johnson? ana mpango gani baada ya kujiuzulu?

• AFP

Kufuatia kuporomoka kwa kishindo kutoka kwa heshima na madaraka, wengi wanajiuliza kile ambacho Waziri Mkuu wa Uingereza anayeondoka, Boris Johnson, atafanya.

Je, atapanga kurudi bunge au atatulia na kupanga kisasi akiwa mchambuzi wa siasa?

Johnson, 58, alikamilisha jukumu lake la mwisho kama Waziri Mkuu katika Bunge kwa kuambia Wabunge: "Hasta la vista, baby" (Hadi tutakapoonana tena). Huenda pia angetumia msemo kutoka kwa filamu ya "Terminator" - "Nitarudi", kwa sababu kauli hiyo ilizua minong'ono kuwa hajamalizika kisiasa.



Washirika wake walisema anataka kuongoza chama cha Conservative katika uchaguzi mkuu miaka miwili ijayo, hata ingawa kiongozi mpya ataapishwa Septemba 5. "Ninashuku hajaacha kabisa wazo la kurudi katika siasa," Profesa wa Siasa, Tim Bale, akaambia AFP.

kurunzi ya Dunia

HATUA YA GHAFLA YA IDARA YA HAKI



Aliyekuwa Rais wa Amerika Donald Trump, wakati wa mkutano wa wanawake wafanyabiashara katika Ikulu ya White House, mjini Washington DC, Machi 27, 2017. PICHA I AFP

# UVAMIZI KWA TRUMP

*Hatua ya kijasiri yatumbukiza Amerika katika hali ambayo haijazoea baada ya makachero wa FBI kuendesha uchunguzi kuhusu kuondolewa na kuhifadhiwa kwa habari muhimu za ulinzi na kufichwa kinyume cha sheria kwa rekodi za serikali.*

• AFP

Uvamizi wa ghafla wa FBI katika nyumba ya kifahari ya Donald Trump, jimbo la Florida, ulitokana na uchunguzi wa masanduku 15 ya rekodi zilizokuwa zimesalimishwa na rais huyo wa zamani ambazo zilijaa habari za siri kuu - ikiwemo kuhusu duru za ujasusi wa binadamu.

Katika hati kiapo ambayo FBI ilitumia kutetea uvamizi huo wa Agosti 8, katika makao ya Trump ya Mar-a-Lago, shirika hilo lilisema lilikuwa likifanya uchunguzi wa uhalifu kuhusiana na "uondoaji usiofaa na uhifadhi wa habari muhimu" na "kuficha rekodi za serikali kinyume cha sheria."

Hati kiapo ya FBI ilianika sababu za kupewa idhini na Jaji wa Florida kufanya uvamizi wa kwanza kuwahi kutekelezwa katika nyumba ya rais wa zamani, hatua ambayo iliibua dhoruba ya kisiasa katika nchi ambayo imegawanyika vibaya.

Trump, anayewazia kugombea urais tena mwaka wa 2024, alilaumu Idara ya Mahakama na Rais Joe Biden, wa chama cha Democratic kwa "kumuandama" na akasema jaji huyo "hangeruhusiwa kuvunja na kuingia katika boma langu."

Kulingana na hati kiapo hiyo, FBI ilianza uchunguzi baada ya Makavazi ya Taifa na Usimamizi wa Rekodi (Nara) kupokea masanduku 15 ya rekodi mnamo Januari 2022 ambayo yalikuwa yameondolewa kinyume cha sheria katika Ikulu ya White House na kupelekwa Mar-a-Lago.

Ilisema kwamba habari muhimu za Ulinzi wa Taifa zilitolewa kutoka rekodi hizo zikiwemo stakabadhi 67 ambazo hazikufaa kufichuliwa, 92 zilizotajwa kuwa za siri na 25 zilizotajwa kuwa za siri kuu.

Miongoni mwa stakabadhi hizo ni habari za kijasusi kutoka kwa "duru za siri za binadamu" kumaanisha zilitoka kwa makachero na majasusi na ni miongoni mwa siri za serikali zinazofichwa sana.

"Siri kuu zilitolewa, zikachanganywa na rekodi zingine na kutambuliwa isivyofaa," kulingana na hati kiapo hiyo. "Baadhi ya stakabadhi hizo zina kile kinachoonekana kuwa maandishi ya mkono (ya Trump)."

Mnamo Juni, kulingana na hati kiapo hiyo, Idara ya Haki ilimwarifu wakili wa Trump kwamba Mar-a-Lago "haikuwa imeidhinishwa kuweka habari za siri."

Walipovamia nyumba ya Trump katika Palm Beach miezi miwili baadaye, maafisa wa FBI walitwaa mabunda ya stakabadhi zaidi zilizotajwa kuwa "Siri Kuu, "Siri" na "zisofaa kufichuliwa."

Kwenye barua aliyoandikia Idara ya Haki mnamo Mei 25 2022, ambayo ilitolewa pamoja na hati kiapo hiyo, wakili wa Trump alisema kwamba huenda habari za siri "ziliwekwa bila kujua miongoni mwa masanduku yaliyopelekwa Mar-a-Lago na waliyohamisha."

Wakili huyo, Evan Corcoran, alisema Trump alikuwa "ameshirikiana kwa hiari" na ombi la Nara kwamba rekodi hizo zirudishwe na akasema kwamba uchunguzi wowote haufai "kuhusisha siasa."

**Rekodi za siri kuuzilitwaliwa na kutotambuliwa ipasavyo. Baadhi ya stakabadhi pia zilihusisha kinachoonekana kuwa barua zilizoandikwa na Trump.**

Corcoran alisema rais ana "mamlaka yote ya kuachilia stakabadhi" na "sheria ya uhalifu inayosimamia uondoaji na uhifadhi wa stakabadhi kinyume cha sheria haitumiki kwa rais."

Mawakili wa serikali walikuwa wamepinga kuachiliwa kwa hati kiapo hiyo lakini jaji akaagiza itolewe na Idara ya Haki, ila sehemu muhimu za kulinda uchunguzi unaoendelea kuhusu usalama wa taifa ziondolewe.

Kwa mfano, sehemu zilizoondolewa katika hati kiapo hiyo ya kurasa 38 ni pamoja na kutolewa kwa majina ya waliotajwa na Idara ya Haki kuwa "idadi kubwa ya raia ambao ni mashahidi."

"Iwapo majina ya mashahidi yatafichuliwa, wanaweza kuwekwa kwenye hatari ikiwemo kulipizwa kisasi, kutishwa au kunyanyaswa na hata vitisho kwa usalama wa mili yao," Idara ya Haki ilisema.

Kibali cha kusaka nyumba ya Trump, ambacho kiliidhinishwa na Mwanasheria Mkuu, Merrick Garland binafsi, kiliruhusu FBI kufanya msako katika "ofisi 45" – kumaanisha ofisi ya kibinafsi ya rais wa 45 wa Amerika katika Mar-a-Lago – na vyumba vya kuhifadhi bidhaa.

Kibali kilisema kwamba kilihusu "uzuiaji maksudi wa habari za ulinzi wa taifa" makosa chini Sheria ya Ujasusi na uwezekano wa "kuzuia uchunguzi." Mbali na uchunguzi kuhusu biashara zake jijini New York, Trump pia anakabiliwa na uchunguzi kuhusu juhudi zake za kubadilisha matokeo ya uchaguzi wa Novemba 2020 na uvamizi katika Bunge la Amerika mnamo Januari 6, 2021 uliotekelezwa na wafuasi wake.

TANZIA

ALIFUFUA UHUSIANO MWEMA WA URUSI NA AMERIKA

# BURIANI GORBACHEV!

*Kuna watu wengi nchini Urusi waliomkashifu kwa jinsi alivyotawala nchi hiyo. Hakuwa mkamilifu. Na hakuna kiongozi mkamilifu. Lakini huyu ni mtu aliyejali sana jinsi ya kuzuia Vita vya Tatu vya Dunia.*

● Na STEVE ROSENBERG, BBC

Ni Machi 2013 na ninamhoji Mikhail Gorbachev katika ofisi zake za utafiti jijini Moscow. Baada ya saa moja na nusu, kiongozi huyo wa zamani wa Urusi anasema 'Vsyo!' ('Hayo ni yako!'). Anasimama, lakini haonekani kuwa na haraka ya kusema kwaheri. Kwa hivyo, tunaendelea kupiga gumzo.

Gorbachev alikuwa amemaliza kuchapisha kitabu cha mwisho cha maisha yake, ambacho alitunukia marehemu mkewe Raisa. Alifariki kutokana na leukaemia mwaka wa 1999. Walikuwa wameoana kwa karibu miaka 46 na kutokana na alivyomsifia, ni wazi kuwa Gorbachev alimkosa sana. Ananionyesha kitabu hicho. Ukurasa wa kwanza unaonyesha nukuu kutoka shajara ya Gorbachev, mwaka mmoja baada ya kifo cha Raisa. "Maisha yangu yamekosa maana yake halisi," aliandika. "Sijawahi kuhisi upweke mkuu kama huu." Lakini macho ya Gorbachev yanaangaza anaponionyesha picha za Raisa katika kitabu hicho: picha wakiwa likizoni, picha za familia, picha akiandamana naye katika ziara za kikazi ng'ambo. Na picha mbili zake anazopenda zaidi: Za


Mikhail na Raisa kabla ya siku ya harusi yao mwaka wa 1953. Wanaonekana kama wachezaji sinema wa Hollywood.

Mimi na Gorbachev tulipokuwa tukitazama kitabu, mpiga picha wetu, Rachel, alikuwa akitazama kinanda katika kona moja ya chumba hicho. "Unaweza kucheza kile?" anauliza Gorbachev. "Sina haja ya kufanya hivyo, kinajicheza chenyewe!" anajibu. Sote tunacheka. Lakini si mzaha. Gorbachev anakikaribia, anakibonyeza na kinanda kinaanza kucheza chenyewe.

"Hiyo ni Chopin," anasema, akitabasamu na anajifanya kama anacheza muziki mwenyewe. Kisha anakigusa na kinanyamaza. "Unaweza pia kukicheza kama kinanda cha kawaida," anasema. "Je, mmoja wenu anaweza kukicheza?" anauliza. Ninamwambia kwamba ninaweza. "Tafadhali keti chini, cheza kitu," anasema Gorbachev.

Sikutarajia hilo. Nililazimika kufikiri kwa haraka. Nitacheza nini? Ni mdundo gani ambao kiongozi huyo wa zamani wa nchi yenye uwezo mkubwa atapendezwa nao. 'Turudi USSR', pengine? Au 'Asante kwa Kukumbuka'? Ninaamua kuwa mwangalifu na kucheza 'Moscow Nights'. Na ninapocheza, jambo ambalo halikutarajiwa linatokea. Gorbachev anaanza kuimba. Na anajua kuiba ,... kwa mdundo. Tunafika tamati na nimamuuliza wimbo mwingine anaopenda. Gorbachev anaomba kibao cha zamani wakati wa vita vya Urusi,

'Dark Is The Night'. Kinazungumzia mwanajeshi kwenye mstari wa mbele katika uwanja wa vita anayefikiria kuhusu mke wake mpenzi aliyemuacha nyumbani. "Katika usiku wenye giza," anaimba Gorbachev, "Ninajua kwamba wewe, mpenzi wangu, umeamka, "Unaketi ukipanguza chozi kwa siri; "Ninapenda macho yako ya kuvutia, "Ningetaka kukupiga busu mdomoni."



Picha ya kiongozi wa mwisho wa Muungano wa Sovieti. PICHA | AFP

Nilikutana na Gorbachev mara ya kwanza Mei 1996, zaidi ya miaka minne baada ya kusambaratika kwa USSR. Alikuwa akijaribu kurudi katika siasa na kupinga Boris Yeltsin katika uchaguzi wa urais Urusi.

Katikati ya miaka ya themanini, Gorbachev alikuwa ameingia katika siasa kwa wito wake wa perestroika (kujenga upya) na glasnost (uwazi). Alikuwa aina ya kiongozi wa Urusi ambaye ulimwengu haukuwa umeona. Alikuwa mchanga, mtulivu. Alionekana kujitolea kujenga uhusiano bora na mataifa ya Ulaya na Amerika na kutia nguvu uchumi wa Urusi uliokuwa umekwama.

Kufikia wakati aliondoka ofisini, Muungano wa Sovieti haukuwepo. Katika uchaguzi wa 1996, Gorbachev alipata asilimia 0.51 ya kura. Alikuwa amepoteza mamlaka - na alishindwa kuyarudisha. Lakini kuna kitu alichobaki nacho: utani wake.

Mwezi uliofuata, mpigaji picha niliyekuwa naye wakati wa kumtembelea Gorbachev alihamishwa kutoka Moscow.

Victor Cooper ni mtu aliyependa maisha, kutoka Texas, ambaye alifanya kila mtu karibu naye kutabasamu. Hakuwa amefahamu lugha ya Urusi vyema lakini moja ya sentesi chache alizokuwa amefahamu ilikuwa: "Samoe glavnoe eto kooritsa!" maana yake "Kitu muhimu zaidi ni kuku!"

Ilimsaidia sana. Kila wakati Victor alipösimamishwa na polisi wa trafiki Moscow, angeteremsha kioo cha dirisha la gari lake na kutamka kwa lafudhi ya kikwao Texas kwamba "Kitu muhimu zaidi ni kuku!" Afisa wa polisi, bila kuelewa alichosema, angemwambia aondoke.

Kazini, nilipewa kazi ya kutayarisha "video nzuri ya kusema kwaheri" kwa Victor ikiwa na jumbe za heri njema kutoka kwa marafiki na wafanyakazi wenzetu Moscow. Kwa kujaribu tu, nilimpigia simu msaidizi wa Gorbachev.

Je, Rais Gorbachev anaweza kukubali kuchangia ujumbe wa video? Jibu lilijiri haraka: "Atafanya hivyo." Nikiwa na mpiga picha mwingine, nilienda katika ofisi ya Gorbachev. "Unataka niseme nini?" aliuliza. Nilitaja kwamba Victor alifahamu kuhusu kuku wa Urusi.

Gorbachev aligeukia kamera na kurekodi ujumbe wake wa kugusa moyo bila kukatiza ambao ulijumuisha maneno haya: "Victor, unavyojua vyema, kitu muhimu zaidi ni kuku!"

Sikuweza kuamini mwenyewe, Gorbachev, aliyekuwa wakati mmoja mtu mwenye nguvu zaidi ulimwenguni, alikuwa amesifu kuku. Victor alipoona video hiyo, alishangaa na kuguswa zaidi. Alikuwa Gorbachev tofauti kabisa na niliyekutana naye 2019. Hayo yalikuwa mahojiano ya tano na ya mwisho kufanya naye. Alikuwa na huzuni ambayo sijawahi kumuona nayo awali. Ni kama kwamba alihisi mafanikio yake yalikuwa yakiharibiwa; kwamba Urusi ilikuwa ikikumbatia udikteta. Gorbachev hakuwa mkamilifu. Hakuna kiongozi aliyekamilika kamwe. Lakini huyu ni mtu aliyejali sana kuhusu kuzuia Vita vya Tatu vya Dunia.

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep




**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*

# EVOLVE

KENYA TOP 100 MID-SIZED COMPANIES
Business Daily KPMG

## BECAUSE YOUR BUSINESS DOESN'T STAND STILL – IT EVOLVES

Each stage of your business cycle presents its own set of opportunities and challenges. Do you have what it takes to be successful at each stage? Enter the 2022 Top100 Midsized Companies Survey and take your seat among the great.

**Benefits:**

- Recognition for companies that have successfully redefined their business and remained agile in an increasingly uncertain business landscape.
- Access to an industry benchmarking report and thought leadership to all participating companies.
- Opportunities to network with peers and sponsors through the exclusive Top100 Mid-Sized Companies conference and gala dinner.
- Winners will be eligible to use the 2022 Kenya Top100 Mid-Sized Companies Club logo.

Survey closes on 9 September 2022


**Submit your entry at: www.eastafricatop100.com**

**Kenya100@kpmg.co.ke**

**020 280 6000**







**Be seated among the great.**

Business Daily KPMG

In partnership with:

IFC International Finance Corporation WORLD BANK GROUP
*Creating Markets, Creating Opportunities*

#Top100KE Top100SME @Top100SME